# Nipashe

Ijumaa Desemba 13, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580100

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

ARIGATOU INTERNATIONAL GNRC

CEFA

2155447/02




## Daktari aeleza athari za kiafya kutokunywa maji

UK. 3

# Mbowe atoa hadhari uchaguzi mkuu 2020

**Aonya** yakitokea kama ya Serikali za Mitaa UN itahusika, Mdee alia uwakilishi mdogo wanawake *...Uk. 2*



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli, akiwa na Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, Rais Ali Mohamed Shein, Katibu Mkuu, Dk. Bashiru Ally katika picha ya pamoja na viongozi wengine baada ya kikao cha ufunguzi wa Majadiliano na Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) jijini Mwanza jana. **PICHA: IKULU**


## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**PINDA ATAMANI JPM AONGOZE HADI 2030**
WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ameeleza kufurahishwa na utendaji wa Rais John Magufuli, akiweka wazi kuwa anatamani aongoze hadi mwaka 2030.

UKURASA WA 3

**MFUNGWA MWINGINE ALIYESAMEHEWA NA RAIS ADAIWA KUIBA**
MFUNGWA mwingine aliyesamehewa na Rais John Magufuli anashikiliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Pwani akidaiwa kuiba ng'ombe ...

UKURASA WA 4

**NDEGE ILIYOKAMATWA CANADA YAACHIWA**
RAIS John Magufuli amesema ndege ya serikali Bombadier Q400, iliyokuwa ...


## MAALIM SEIF AWAPONZA MA-RPC

UK.3

# Wakuu, bodi za taasisi 196 za umma kikaangoni

UKURASA 2


MICHEZO **SAMATTA: SABABU KIPIGO NAPOLI HII** UK.31

MAONI, KATUNI UK.6

# Pinda atamani JPM aongoze hadi 2030

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, ameeleza kufurahishwa na utendaji wa Rais John Magufuli, akiweka wazi kuwa anatamani aongoze hadi mwaka 2030.

Pinda aliyasema hayo jana jijini Mwanza wakati Rais Magufuli alipofungua semina ya wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (NEC).

Akizungumza mbele ya Rais Magufuli, Pinda alisema: "Kwa miaka mingi umefanya kazi hizi, lakini ninapata matumaini makubwa sana kwamba miaka hii 10 uliyopewa itatupeleka pazuri sana.

"Ni kwa kuwa Katiba zenyewe zinabana, lakini kama siyo kwa sababu hiyo, walah ningesema 'mzee piga miaka mingine, ongeza kama mitano tu'.

"Ninajua hata mkijaribu kumshawishi atawakatalia tu, lakini nataka niseme kwa namna ninavyoguswa na kazi kubwa unayoifanya, ni matumaini yetu katika kipindi hiki kama utatugomea kuongeza kidogo lakini utahakikisha unatupa kiongozi mwingine mzuri kwa kusaidiana na NEC, atakayeweza kusukuma mawazo haya na maamuzi haya magumu ambayo unayafanya."

Pinda pia aliwaomba wajumbe wa NEC kuunga mkono juhudi hizo kwa kuwa nchi ina uwezo mkubwa kama wote watakwenda kwa lugha ya Mwenyekiti wa CCM na kutenda kama anavyotaka watende, itakuwa na mafanikio makubwa ndani ya kipindi kifupi.

**JPM AIONYA CCM**

Kwenye hotuba yake, Rais Magufuli aliitahadharisha CCM kuhusu anguko la vyama vilivyopigania uhuru barani Afrika, akieleza kuwa vingi vimejisahau na kuendesha nchi kwa mazoea.

Alisema CCM kimefanikiwa kushika hatamu za uongozi katika kipindi cha miaka 58 ya uhuru wa Tanzania na kitaendelea kuongoza endapo kitakidhi mahitaji na matarajio ya wananchi.

"Siku mbili zilizopita, tumesherehekea maadhimisho ya miaka 58 ya uhuru wa Tanzania Bara, katika miaka

INAENDELEA UK. 8

# Mbowe atoa hadhari uchaguzi mkuu 2020

**Na Enock Charles**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, ametoa tahadhari kwa serikali kuhusu uchaguzi mkuu ujao.

Amedai iwapo serikali itashindwa kudhibiti rafu dhidi ya upinzani kama ilivyokuwa katika uchaguzi uliopita wa serikali za mitaa, nchi itaingia katika machafuko ambayo anaamini yatalazimika kusuluhishwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN).

Kiongozi huyo wa chama kikuu cha upinzani nchini, alitoa kauli hiyo jana alipozungumza katika mkutano mkuu wa Baraza la Wanawake wa chama hicho (Bawacha) jijini Dar es Salaam.

Alidai chama hicho kimejipanga kukabiliana na aina zote za hujuma zilizopangwa kufanyika katika Uchaguzi Mkuu mwakani.

"Kama serikali inafikiri inaweza kufanya kile kilichofanyika katika uchaguzi wa serikali za mitaa, basi mpatanishi wake atakuja kuwa Katibu Mkuu wa UN," Mbowe alitahadharisha.

Ingawa kiongozi huyo wa Chadema hakufafanua zaidi kuhusu rafu alizokusudia, vyama kadhaa vya upinzani vilitangaza kujitoa katika uchaguzi uliopita wa serikali za mitaa, vikilalama kuenguliwa kwa wagombea wake katika mchakato wa kuwania uongozi katika ngazi mbalimbali.

Katika mkutano wa jana, Mbowe pia alivunja ukimya kuhusu wanaopinga kuendelea kwake kuwania nafasi ya uenyekiti wa Chadema, akieleza kuwa anawashangaa kwa kuwa kila mwanachama wa chama hicho anayo fursa ya kuwania nafasi hiyo.

Mbowe pia alitumia nafasi hiyo kueleza kuwa wanajipanga kukibadilisha chama hicho kutoka katika mfumo wa analojia kwenda katika mfumo wa kidigitali.

"Tutazindua mfumo wa digitali (Chadema Digital), katika 'information system' (mfumo wa taarifa) ya chama, kila kitu kitafanyika kidigitali, zikiwamo taarifa za chama na kampeni zetu," Mbowe alisema na kuahidi kuwa chama kimepanga kuzindua mfumo huo Desemba 18, mwaka huu. Alisema iwapo wanachama milioni sita wa chama hicho watakichangia chama, kitakusanya Sh. bilioni 12 ambazo zitasaidia katika kampeni za uchaguzi mkuu mwakani.

Mbowe pia aliwaonya wanaogombea wa nafasi za uongozi ndani ya Bawacha kuhusu kile alichodai kuwa wengi wamekuwa wakipambana kuingia ndani ya baraza hilo ili kupata fursa za ubunge na udiwani wa viti maalum.

Mwenyekiti wa baraza hilo na Mbunge Kawe, Halima Mdee, alisema wanawake bado wana vikwazo vingi ikiwamo uwapo wa uwakilishi hafifu katika nafasi za uongozi, hali ngumu ya kiuchumi na unyanyasaji wanaopata kutoka kwa wanaume.

"Kwa mfano, katika wabunge 260 wa kuchaguliwa, wanawake ni 26 ambayo ni asilimia 10 kwa vyama vyote, waliobaki 234, sawa na asilimia 90 ni wanaume, hivyo pamoja na juhudi kubwa zinazofanyika, bado uwakilishi wa wanawake si wa kuridhisha," alisema.

Mdee aliahidi kuendelea kupigania maslahi ya wanawake nchini na kuhakikisha kunaondolewa aina zote za ukandamizaji dhidi ya wanawake, ikiwa angechaguliwa kuendelea kuliongoza baraza hilo katika uchaguzi uliofanyika usiku wa kuamkia leo.




Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo (kushoto), akizungumza katika ufunguzi wa mkutano wa 11 wa kujadili elimu nchini Tanzania, ulioandaliwa na Taasisi ya Elimu Tanzania, TenMet, unaoendelea jijini Dodoma jana. Mkutano huo umewakutanisha wadau wa elimu kutoka serikalini, mashirika, taasisi za elimu, watafiti wa elimu na asasi za kiraia kujadili ubora wa elimu ya Tanzania. Mkutano huo utamalizika kesho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vigogo, bodi 129 kikaangoni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ZIKIWA zimebaki siku 42 za utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli kwa taasisi, mashirika na kampuni kutoa michango kwenye mfuko mkuu wa serikali, taasisi 129 hadi sasa bado hazijatekeleza agizo hilo.

Novemba 24, mwaka huu wakati akipokea michango na gawio kutoka taasisi za serikali Ikulu Chamwino, Rais Magufuli alitoa siku 60 kwa taasisi ambazo zilikuwa hazijatoa gawio, kuhakikisha zinafanya hivyo kwa kuwa serikali imewekeza fedha ili kupata faida.

Siku hiyo, Rais alipokea Sh. trilioni 1.05 kutoka kwa taasisi 79 kati ya 266 na kuagiza taasisi 187 ambazo hazijatoa kufanya hivyo ndani ya siku 60.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, wakati akipokea michango na gawio kutoka taasisi mbalimbali jana jijini hapa, alibainisha kuwa tangu kutolewa agizo hilo, taasisi 58 kati ya 187 zimetoa jumla ya Sh. bilioni 12.12.

"Novemba 24, kule Ikulu Chamwino, taasisi, kampuni na mashirika yaliyojitokeza yalikuwa 79, (Rais) aliniagiza ndani ya siku 60, taasisi zote ambazo serikali imewekeza, zilete gawio na michango serikali ili fedha hizo tuzitumie kwa maendeleo ya taifa letu," alisema.

"Rais alitumia lugha kali kidogo. Moja, alisema waziwazi pale lakini nyingine alininong'oneza 'waziri acha kuwa mpole', nawakumbusha wote ambao hawajaleta gawio au mchango, ifikapo saa sita usiku Januari 23, 2020, kama hawajaleta gawio wala michango, bodi hizo zimevunjwa," alionya.

Alisema watendaji wakuu wa taasisi husika pia watakuwa hawana kazi na hiyo ndiyo amri ya serikali. "Wale ambao hawajaleta, tukio kama hili litakuwa Januari 23, 2020 kabla ya 'deadline' (ukomo) haijafika saa sita usiku, baada ya hapo nitashusha panga, litapita, nipo tayari kuoga damu," alisema.

Alisema utoaji wa michango na gawio ndiyo njia ya nchi kujitegemea na lazima nchi isonge mbele.

"Narudia tena, Waziri wa Fedha wa Tanzania kwenda kuomba omba huko siyo jambo zuri, tunadhalilika mno huko tunakokwenda.

"Na Rais anatukumbusha kila siku, nchi yetu tajiri, watu zaidi ya milioni 55 hatuwezi kuwa maskini, hakuna kitu Mungu alichotunyima katika taifa letu.

"Tunapowekeza kwenye vyombo vyetu, lazima tuonyeshe jeuri hiyo hiyo, msimpeleke Waziri wa Fedha kwenda kuomba hata kidogo, mpelekeni waziri akakope, ukikopa ni ya kwako cha muhimu utumie vizuri ilimradi ujihakikishie una uwezo wa kulipa, lakini kwenda kuinga bakuli aaah, tufike mwisho," alisema. Waziri Mpango alisema ili awe na jeuri hiyo, ni wajibu wa mashirika kutoa gawio na michango kwa watanzania.

"Naomba kuwahakikishia Watanzania serikali yetu inayoongozwa na Rais Magufuli tutatumia fedha hizi vizuri kwa maendeleo ya Watanzania, watembee kifua mbele," alisema.

Awali, Msajili wa Hazina, Dk. Athuman Mbuttuka, alisema Novemba 25, mwaka huu, waziri alipokea Sh. bilioni 2.75 kutoka taasisi nne na zingine zimeendelea kujitokeza kutoa michango.

**HABARI KITAIFA**



Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima (wa pili kulia), akijadiliana jambo na Ofisa Misitu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Dkt Freddy Manyika. Wengine pichani kuanzia kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa na Hifadhi ya Mazingira (NEMC) Dkt. Samuel Gwamaka na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) Dkt. Agnes Kijazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfungwa mwingine aliyesamehewa na Rais adaiwa kuiba

**Na Romana Mallya**

MFUNGWA mwingine aliyesamehewa na Rais John Magufuli anashikiliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Pwani akidaiwa kuiba ng'ombe mwenye thamani ya Sh. milioni 1.2.

Mustafa Malimi (23), mkazi wa Mikoroshini, Chalinze mkoani Pwani, ni miongoni mwa wafungwa 5,533 waliotoka gerezani Jumanne kwa msamaha wa Rais Magufuli.Tukio la hilo ni la pili tangu Rais Magufuli atangaze msamaha huo, la kwanza lilitokea Jumanne usiku huko Makambako, Njombe baada ya mfungwa Musa Msolwa, maarufu kama Hitler, aliyeachiwa gerezani saa 11 jioni na ilipofika saa tisa usiku akakamatwa kwenye nyumba ya kulala wageni akidaiwa kuvunja ili kujipatia fedha.

Saa chache baadaye, Malimi naye alikamatwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Pwani akituhumiwa kukutwa na ng'ombe wa wizi, mali ya Otaigo Elisha (30), mkazi wa Pera, Chalinze.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema tukio hilo lilitokea juzi saa nne asubuhi maeneo ya Nero, Chalinze. "Malimi alikamatwa akiwa ameiba ng'ombe dume mwenye thamani ya Sh. milioni 1.2 na kumchinja. Mtuhumiwa huyu aliachiwa huru kutoka Gereza la Ubena, Chalinze Jumatatu kwa msamaha wa Rais Magufuli," alidai.

Kamanda Nyigesa alisema Jeshi la Polisi mkoani humo pia linashikilia dereva Baraka Njoka (37), mkazi wa Ubungo Kibo jijini Dar es Salaam kwa tuhuma za kupakia mzigo wa mafuta ya kupikia ambayo hayakulipiwa kodi ya serikali.

Alidai gari lililotumika kubeba mzigo huo ni aina ya Fuso lenye namba za usajili T 582 AWB, ambalo lilikamatwa likiwa limepakia madumu ya mafuta ya kupikia 860 aina ya Mico Gold na OK.

"Jeshi la Polisi mkoani humu likiwa katika operesheni mbalimbali za kuzuia makosa kuelekea mwishoni mwa mwaka, ndipo lilipolikamata gari hili.

"Mafuta haya yalikuwa hayana vibali na yamekwepa kulipa ushuru wa serikali. Dereva na mali iliyokamatwa atafikishwa mahakamani upelelezi ukikamilika," alisema.

# Daktari aeleza athari kiafya kutokunywa maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATU wanaokunywa maji kidogo kulinganisha na kiwango cha chumvi kinachotengenezwa mwilini, wako hatarini kupata mawe kwenye figo na mfumo wa mkojo kwa ujumla, imeelezwa.

Daktari Bingwa wa Mfumo wa Mkojo na Upandikizaji wa Figo katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dk. Remigius Rugakingira, aliyasema hayo alipotoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari wakati wa ziara ya timu ya maofisa habari wa wizara na taasisi zake mkoani Dodoma jana.

Dk. Rugakingira alisema hospitali hiyo tangu kuanzishwa kwake imepokea wagonjwa wengi wenye mawe kwenye mfumo huo, akibainisha kuwa tatizo hilo linawakumba watu wa rika zote.

Alisema awali walikuwa wanapokea wastani wa wagonjwa watano kwa mwezi, lakini kwa sasa si chini ya 32 kwa mwezi, wakitoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.

"Kama unakunywa maji kidogo kulinganisha na aina ya chumvi inayotengenezwa mwilini, una hatari ya kupata mawe, pia kuwa na bakteria wengi katika mfumo wa mkojo, unaweza kutengeneza mawe," alisema.

INAENDELEA UK. 8

# Maalim Seif aponza ma-RPC

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZIARA ya Mshauri wa Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif kisiwani Pemba, imesababisha makamanda wawili wa polisi kisiwani Pemba kushushwa vyeo.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamadi Yusuf Masauni, alitoa agizo la kushushwa vyeo kwa makamanda hao kwa madai ya kushindwa kutekeleza wajibu wao kama walivyoelekezwa na serikali.

Pia Masauni amemuagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kumshusha cheo kimoja Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kusini Pemba, Hassan Nassir, kutokana na kile alichodai kuwa ni udhaifu wa utendaji wa kamanda huyo.

Agizo hilo alilitoa wakati akizungumza na waandishi wa habari, Mjini Magharibi Unguja.

Masauni alisema amefikia uamuzi huo kutokana na makamanda hao wa mikoa yote ya Pemba kuonyesha udhaifu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kazi ikiwamo kuimarisha ulinzi na usalama.

Makamanda walioshushwa vyeo ni wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Sheikhani Mohamedi Sheikhani na Kamanda wa Kusini Unguja, Hassan Nassir Ali.

Masauni alisema kwa muda mrefu haridhishwi na matukio yanayoendelea kisiwani Pemba huku makamanda hao wakiwa kimya bila ya kutoa uamuzi wowote na hivyo kuonyesha dhahiri kwamba wameshindwa na kazi.

Alieleza kuwa Rais John Magufuli, ametoa agizo la kufanyika mikutano ya hadhara, lakini bado wanasiasa wanafanya mikutano hiyo ndani kisiwani Pemba.

"Napata mashaka makubwa na uwezo wa kazi za makamanda hawa, nchi hii hatuwezi kila siku tukawa tuna abudu siasa, wakati wa siasa umepita na viongozi wameshachaguliwa tayari, kwanini makamanda hawa wanashindwa kuzuia mikutano hii ya siasa

INAENDELEA UK. 8


**HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

**MNADA WA UUZAJI WA VIWANJA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote kuwa zoezi la uuzaji wa Viwanja kwa njia ya Mnada litafanyika tarehe **14 Disemba, 2019** siku ya Jumamosi. Mnada utafanyika katika eneo la wazi la Manispaa ya zamani (karibu na Sabasaba) kuanzia saa 4:00 Asubuhi. Zoezi la kutembelea viwanja hivyo litafanyika Ijumaa tarehe 13/12/2019 saa 4:00 asubuhi eneo la mnada. Usafiri utakuwepo.

Viwanja vinavyouzwa ni Maeneo ya:

| ENEO | MATUMIZI NA BEI TSHS KWA (SQM1) |
|---|---|
| IYUMBU (New Town Centre) | • Viwanja vya Nyumba za kupangisha (Apartments)<br>• Viwanja vya Biashara<br>• Viwanja vya Viwanda Vidogo |
| NALA (Industrial Area) | • Viwanja vya Viwanda vya aina mbalimbali |
| NJEDENGWA (Investment Centre) | • Viwanja vya Nyumba za kupangisha (Apartments)<br>• Viwanja vya Biashara |
| NZUGUNI (Jirani na Uwanja wa Mpira, Soko Kuu na Stendi kuu mpya ya mabasi) | • Viwanja vya Hoteli<br>• Viwanja vya Biashara<br>• Viwanja vya Maduka makubwa (Shopping Malls) |

**NB**:

- Asilimia 50 ya Malipo italipwa siku ya Mnada
- Asilimia 50 inayobaki italipwa ndani ya siku 14 baada ya Mnada.

Tangazo hili limetolewa na:
**Mkurugenzi wa Jiji,**
**DODOMA**

# Ndege iliyokamatwa yaachiwa

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amesema ndege ya serikali aina ya Bombadier Q400, iliyokuwa ikishikiliwa Canada, imeachiwa.

Aliyasema hayo jana jijini Mwanza alipofungua semina ya wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Rais Magufuli aliwaeleza wajumbe kuwa: "Kwa taarifa tu ndege yetu iliyokuwa imeshikwa Canada imeachiwa, mtatangaziwa tarehe ya kuipokea na mtaipokea hapa Mwanza," Rais Magufuli alisema.

Novemba 23, mwaka huu, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, akiwa Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma, alitangaza kushikiliwa kwa ndege hiyo Canada.

Prof. Kabudi alisema kumekuwa na hujuma kubwa zinazofanywa na mabeberu kwa lengo la kurudisha nyuma juhudi na maendeleo ya nchi.

Alisema baada ya ndege hiyo kukamatwa, alimwita Balozi wa Canada nchini na kumweleza namna Serikali ya Tanzania inavyokasirishwa na vitendo vya ndege zake kukamatwa nchini humo kila ikifikia hatua ya kurudi Tanzania.

"Limetokea jambo la kusikitisha ambalo ni vyema Watanzania pia walielewe jinsi ambavyo hujuma za kibeberu zinavyofanyika kurudisha kasi ya maendeleo, tena kwa mara ya tatu ndege ambayo ilitakiwa kufika Tanzania, imekamatwa tena Canada na kesi ipo mahakamani.

"Aliyefanya hivyo ni mtu yuleyule aliyekamata ndege yetu Afrika Kusini, tukaenda mahakamani tukamshinda, sasa amekimbilia Canada na amekamata ndege yetu ya Bombadier Q400," alisema.

# Ofisa Takukuru atozwa 500,000/- kudai rushwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wilayani Kahama mkoani Shinyanga, imemtia hatiani Ofisa Uhamiaji wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) wilayani hapa kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 100,000.

Kutokana na kosa hilo, Mahakama imemwamuru Ofisa huyo Cosmas Ntakisigiye Eliud, kulipa faini ya Sh. 500,000.

Ntakisigiye alitiwa hatiani kwa kutenda kosa hilo kinyume cha sheria kifungu cha 15(1)(a) na (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2017.

Ntakisigiye awali alishtakiwa katika kesi ya jinai namba 147/208 kwenye Mahakama ya Wilaya ya Kahama kwa kosa la kuomba rushwa kiasi cha Sh. 300,000 kutoka kwa Bosile Chacha kama kishawishi cha kutochukua hatua dhidi yake kutokana na mashtaka kuhusu uraia wake.

Katika kiasi cha fedha alichodai ofisa huyo wa Uhamiaji kutoka kwa Chacha alijipatia Sh. 100,000 kwa njia ya udanganyifu.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Kahama, Evodia Kyaruzi, alimtia hatiani ofisa huyo kwa kosa la kujipatia kiasi cha Sh. 100,000 kutoka kwa mshtakiwa Chacha.

Hakimu Kyaruzi alimtia hatiani na kumhukumu Ntakisigiye kwenda jela miaka mitatu au kulipa faini kiasi cha Sh. 1500,000.

Aidha, Hakimu Kyaruzi aliwataka wananchi wa Mkoa wa Shinyanga kuendelea kutoa ushirikiano kwa Takukuru kama ambavyo wamekuwa wakifanya ili kuondoa kero ya rushwa katika mkoa huo.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Japhet Justine, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu mafanikio kwa miaka 4 tangu benki ianze kukopesha. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Tanzania yataka hatua udhibiti athari tabianchi

**Na Mwandishi Wetu,** MADRID

TANZANIA imetoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuchukua hatua za haraka na za pamoja kushughulikia suala la mabadiliko ya tabianchi na athari zake.

Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mussa Sima, alitoa wito huo jana wakati wa mkutano wa 25 wa mawaziri wa nchi wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi unaondelea jijini Madrid, Hispania.

Aliwataka wajumbe wanaoshiriki katika mkutano huo kuendelea kuchukua hatua mahsusi za kushughulikia matatizo ya mabadiliko ya tabia nchi. "Tunahitaji kuendeleza kasi ya kushughulikia mabadiliko ya tabianchi kwa kubainisha malengo mahsusi ya kupunguza tatizo hili na kuchukua hatua zote muhimu zinazohitajika," alisema.

Alibainisha kuwa athari za mabadiliko ya tabianchi tayari zimeonekana Tanzania kupitia matukio makubwa ya hali ya hewa ikiwamo mvua kubwa na kuongeza kwa joto, kunakosababisha mafuriko na kusambaa kwa magonjwa ambukizi, upotevu wa mali na maisha ya wanadamu na uharibifu wa miundombinu ya barabara na madaraja katika maeneo mengi ya nchi.

Alisema kwa mujibu wa taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Oktoba mwaka huu, kulikuwa na mvua kubwa kulinganisha na kipindi kingine kama hicho kwa karibu muongo mmoja uliopita na kuathiri sekta zote muhimu, kama vile kilimo, afya, uvuvi, mifugo, maji na afya, hivyo kuongeza kwa magonjwa yakiwamo dengue na malaria.

Sima pia alisema Serikali ya Tanzania, imekuwa ikichukua hatua thabiti ambazo zinachangia katika kupunguza athari za mabadiliko la gesijoto licha ya ukweli kuwa haikuchangia katika chanzo cha tatizo hilo.

Aliuarifu mkutano huo kuwa Tanzania imenunua rada mbili zitakazotumiwa na TMA kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utabiri hali ya hewa na majanga yatokanayo na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema serikali pia inaendelea kupanua na kujenga mtandao wa barabara za mabasi ya mwendo wa haraka katika Jiji la Dar es Salaam; inajenga reli ya viwango vya kimataifa (SGR) na Bwabwa la Mwalimu Nyerere ambalo litazalisha MW 2115.

"Utekelezaji wa miradi hii siyo tu unachochea maendeleo ya taifa na ukuaji wa uchumi, bali unachangia pia katika upunguzaji wa gesijoto ambazo zinasabaisha ongezeko la joto la dunia ambalo husababisha mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Pamoja na hayo, Sima pia aliuarifu mkutano kuwa, Tanzania imedhamiria kuendelea kuongeza maeneo yanayonyonya gesijoto na kutunza uoto wa asili kwa kuwa na eneo la misitu lenye ekari takriban milioni 48, kuendelea kuongeza eneo ambalo limehifadhiwa kwa kuongeza idadi ya hifadhi za taifa na kuendelea na kampeni ya upandaji miti nchi nzima.

Alitoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuunga mkono jitihada za Tanzania katika kushughulikia suala la mabadiliko ya tabianchi na kuziomba nchi zilizoendelea kuongeza juhudi zaidi katika kushughulikia suala la mabadiliko ya tabianchi kwa kutekeleza miradi na kutoa fedha na teknolojia kwa ajili ya kushughulikia tatizo hilo.

Ujumbe wa Tanzania katika mkutano huo ulioanza Desemba 2, ukitarajiwa kuhitimishwa leo, unaongozwa na Sima. Mkutano huo unahudhuriwa na washiriki zaidi 20,000 kutoka serikali za kitaifa, majimbo, majiji na halmashauri, asasi za kiraia, sekta binafsi na jumuiya ya wafanyabiashara.

Mkutano huo una ajenda ya kujali utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi na makubaliano ya Paris kuhusu mabadiliko ya tabianchi.



Kupitia kampeni ya Kibiashara Zaidi ya East Africa Television na East Africa Radio, Mkurugenzi wa Kampuni ya Canghui Traders LTD, Dennis Jerry (kushoto), akifanyiwa mahojiano na mtangazaji Samson Charles, ambapo alieleza juu ya ubora wa samani na vifaa vya ujenzi wanavyouza na jinsi ambavyo wamefika katika maeneo mbalimbali Tanzania. **PICHA: EATV**

# Kigogo chama cha siasa mbaroni kwa tuhuma rushwa milioni 50/-

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imemtia mbaroni Katibu Mkuu Chama Cha Kijamii (CCK), Renatus Muabhi, akituhumiwa kujifanya mtumishi wa taasisi hiyo na kuomba rushwa ya Sh. milioni 50.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Ilala, Christopher Myava, alidai Muabhi aliomba rushwa hiyo kwa Manraj Bharya ambaye ni Mkurugenzi wa Bharya Engeneering and Constructing Company (Becco) iliyoko Vingunguti jijini.

"Uchunguzi wa Takukuru umebaini Muabhi alikuwa na dhumuni la kuomba rushwa hiyo ili amsaidie Bharya katika tuhuma zilizokuwa zikimkabili Independent Power Tanzania Limited (IPTL)," alidai. Myava alidai mtuhumiwa huyo alikamatwa Desemba 10, mwaka huu, akiwa katika ofisi za Kampuni ya Bharya, akiwa amepokea fedha za mtego wa rushwa Sh. milioni moja.

"Uchunguzi ukikamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake," alisema.

Myava alibainisha kuwa katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Juni mwaka huu, Takukuru ilipokea malalamiko 242.

Aliitahadharisha jamii kuelekea kipindi cha mwisho wa mwaka kuwa kunakuwa na matukio mengi ya utapeli na watu kujifanya watumishi wa taasisi nyeti za serikali ili kujipatia fedha.

# TRC yajivunia mafanikio uongozi wa Magufuli

**Na Juster Prudence**

SERIKALI ya awamu ya tano, imeleta mchango mkubwa katika kukamilisha na kuleta mafanikio katika sekta ya reli nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa uongozi wa Rais John Magufuli umekuwa wa kipekee kutokana na mafanikio na malengo aliyoyafikia katika sekta ya reli.

Kwa mujibu wa Kadogosa, serikali imesaidia kuunganisha TRC iwe moja ambapo awali kulikuwa na mashirika mawili RAHACO na TRL ambayo yameungana na kutengenea bodi moja ya TRC inayosaidia katika usafirishaji ukizingatia kabla njia na uendeshaji vilikuwa na wamiliki tofauti.

Aidha, uwezo wa treni za kubeba mizigo kwa mwaka umeongezeka, na kwa takwimu zilizopo mwaka 2016-2017 treni ilibeba jumla ya tani 293,000, mwaka 2017-2018 ilibeba tani 366,000 na kwa mwaka 2018-2019 treni imebeba jumla ya tani za mizigo 426,000 na kuongeza kuwa treni za kubeba abiria kwa mwaka huu zimebeba abiria 556,000 ukilinganisha na ilivyokuwa mwaka 2015, ambapo kwa mwaka kulikuwa na abiria 385,000.

Kadogosa alisema serikali ya awamu ya tano pia imeongeza mapato yake kupitia TRC kutoka Sh. bilioni 15 iliyokusanywa mwaka 2015 hadi Sh. bilioni 45.5 ambazo zimekusanywa mwaka huu.

Alisema Shirika la Reli limeamua kuongeza safari kutoka Dar es Salaam mpaka Moshi ambazo zitaanza kuanzia wiki ijayo, hivyo treni itakuwa ikisafirisha abiria mara tatu kwa wiki.

Jambo jingine lililofanywa na serikali ni ukarabati wa mabehewa ambapo hivi karibuni Rais Magufuli alitoa Sh. bilioni 5 kwa ajili ya ukarabati huo na mpaka sasa jumla ya mabehewa 150 yakiwamo ya mizigo na abiria yamerekebishwa, huku mengine yakisubiri vifaa maalum kutoka nje ya nchi.

Kadogosa alisema kuna mradi mikubwa miwili inayoendelea ambayo ni ujenzi wa njia ya kati ambao umekamilika kwa asilimia 70 na mpaka sasa, ujenzi wa reli kutoka Dar es Salaam hadi Isaka utakaosaidia kuzihudumia nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Aidha, alieleza juu ya ujenzi wa reli ya kisasa ambao ni mradi wa pili umekamilika kwa zaidi ya asilimia 70 mpaka hivi sasa na muda si mrefu mradi huo utakamilika, na kuongeza kuwa reli ya kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro ambayo imegharimu Sh. bilioni 2.7 mpaka sasa umekamilika kwa zaidi ya asilimia 72, huku ujenzi wa reli kutoka Morogoro-Makutupora ukikamilika kwa asilimia 42.

Alisema miradi hiyo imeleta fursa na kutoa ajira kwa watu wengi nchini ikiwamo wafanyakazi zaidi ya 14,000 ambao asilimia 88 ni Watanzania pamoja na makandarasi ambao asilimia 52 pia ni Watanzania, asilimia 48 wakiwa wa kutoka nje.



# Pinda atamani JPM aongoze hadi 2030

INATOKA UK. 2

hii yote, CCM ndicho kimeshika madaraka ukiacha miaka michache ya uongozi wa vyama mama vya TANU na ASP.

"Hivyo, kimsingi tangu tumepata uhuru, CCM imeshika hatamu za uongozi kwa kipindi chote hiki jambo ambalo ni nadra katika nchi nyingi za Afrika. Kwa hakika, hili ni jambo la kujivunia na kujipongeza sisi wote," alisema.

Aliongeza kuwa ni miaka minne tangu chama hicho kishike hatamu za uongozi wa serikali ya awamu ya tano na umesalia mwaka mmoja kukamilisha kipindi cha miaka mitano. "Lakini, nina uhakika kila mjumbe aliyepo hapa, angependa chama chetu kiendelee kushika hatamu za uongozi miaka mingine ijayo. Na hilo litawezekana tu, endapo tutaweza kukidhi mahitaji na matarajio ya Watanzania," alisema. Rais Magufuli pia alisema serikali yake inakabiliwa na vikwazo kadhaa ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa utayari kwa baadhi wananchi na viongozi kukubali na kuendana na mabadiliko.

"Bado watu wanashindwa au wanachelewa kuelewa kuwa tupo kwenye zama mpya ambapo nia yetu kubwa ni kujenga taifa linalojitegemea kiuchumi.

"Hawajaelewa kwamba ni lazima tujenge nidhamu na uadilifu katika kazi na kuelekeza rasilimali zetu kwenye mikakati ya maendeleo inayolenga kuleta ukombozi kiuchumi," alisema.

Rais Magufuli alitaja vikwazo vingine kuwa ni hujuma dhidi ya jitihada za serikali zinazofanywa na baadhi ya watu wasiwo itakia mema nchi.

Alisema hujuma hizo zinalenga kufifisha jitihada za kujikomboa kiuchumi kwa maslahi yao binafsi na watu hawataki kuona udhibiti wa rasilimali za nchi ambazo walikuwa wakizivuna na kusafirisha wanavyotaka bila kuulizwa na mtu.

Alisema wanatumia kila njia kufifisha jitihada za serikali na kupenyeza ajenda zao na wakati mwingine, wanatumia Asasi za Kiraia (Azaki) na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na kujifanya wanafundisha demokrasia na haki za binadamu, ilhali wao wenyewe wanavunja misingi hiyo kwa kujenga mifumo ya kinyonyaji, kuchochea machafuko na kuingilia uhuru wa mataifa mengine.

"Wakati mwingine, watajenga mazingira ya taharuki na kusema ebola imeingia Tanzania ilimradi tu ionekane nchi haiko salama.

"Inatupasa tutambue kuwa hii ndiyo changamoto (tatizo) kubwa katika mapito yetu kuelekea ukombozi wa kiuchumi; na tusiposimama imara na kujenga uzalendo na moyo wa kujitolea kwa taifa, hatuwezi kushinda.

"Ni lazima tujitambue, tujue tulipotoka, mahali tulipo na mwelekeo wetu kwa manufaa ya Watanzania," Rais Magufuli alisema.




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli (TRC), Masanja Kadogosa, akizugumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu miaka minne ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano katika sekta ya miundombinu ya reli. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Maalim Seif aponza ma-RPC

INATOKA UK. 3

ambayo inaendelea kufanywa na huyu anayeitwa mshauri wa Chama cha ACT-Wazalendo," alihoji Masauni.

Maalim Seif yupo kisiwani Pemba katika ziara za kuimarisha chama chake kuelekea katika uchaguzi wa ndani pamoja na uchaguzi mkuu mwakani.

Masauni alisisitiza kuwa makamanda hao wanatakiwa kuondolewa kwenye nafasi walizokuwa nazo na si kupangiwa katika mikoa mingine.

Hata hivyo, alisema kwa utendaji kazi wao hawawezi kuivusha nchi salama katika kipindi kijacho cha uchaguzi mkuu 2020. Masauni alieleza kuwa sababu nyingine ni kushindwa kukamilisha ujenzi wa nyumba za makazi za jeshi la polisi ndani ya kisiwa hicho licha serikali kutoa fedha pamoja na vifaa vya ujenzi wa nyumba hizo.

Katika hatua nyingine Masauni alisema kuwa kila Kamanda wa Jeshi la Polisi nchini anapaswa kutekeleza agizo linalotolewa na serikali pamoja na Amiri Jeshi Mkuu.

Wakizungumza na Nipashe makamanda hao walioagizwa kuondolewa kwenye nafasi zao, walisema bado hawajapokea agizo lolote kutoka kwa wakubwa wao na hali ya amani kisiwani Pemba imetawala.

# Daktari aeleza athari kiafya kutokunywa maji

INATOKA UK. 3

Alibainisha kuwa tatizo hilo ni kwa wanaume na wanawake, lakini linategemea na mhusika anakunywa maji kiasi gani na mkojo unatoka kiasi gani.

"'Nature' ya mawe ambayo tunayaona ni magumu na tuna historia hapa tulitoa jiwe lenye sentimita 4.5 ambalo tumetoa kwenye kibofu, na sentimita 2.6 ambalo limetolewa kwenye figo," alisema.

"Tumeweza kufanyia upasuaji mtoto wa miaka minne alikuwa ana jiwe kubwa kwenye njia ya mkojo, leo (jana) nimemtoa mtu mwenye umri wa miaka 96, alikuwa na jiwe kwenye njia ya mkojo," alisema.

Daktari huyo alisema mashine ya kusaga mawe hayo itafungwa mwezi ujao kwenye hospitali hiyo na itakuwa ya kisasa na mfumo mzima umegharimu takriban Sh. bilioni sita.

"Uwekezaji wa mashine hii ni mkubwa na wa kisasa, ni sawa na Ujerumani na nchi zinginge, itatumia mionzi, mfumo utakuwa unatumia kamera, unaenda kwenye eneo la jiwe na kulivunja, na njia nyingine ya pili ni kutumia mfumo wa kufungua," alisema. Alisema kuna wagonjwa kutoka nchi za Comoro, Saudi Arabia, Ghana na Uganda wamefanyiwa upasuaji wa kuondoa mawe.

Alipoulizwa kuhusu gharama, daktari huyo alisema gharama ya kutibu tatizo hilo ni kubwa, lakini katika hospitali hiyo gharama yake inahimilika.

"Tunasita sana kuzungumzia suala la gharama maana mtu unamwambia Sh. milioni moja au mbili anaona 'eeh Mungu wangu, naenda kufa!' Wakati ukipiga gharama za nje ya nchi ni kubwa," alisema.

Mtaalamu huyo alisema mtu ambaye jiwe limesagwa, ataruhusiwa siku hiyo hiyo, lakini aliyefanyiwa upasuaji, atakaa hospitali kwa kipindi cha kuanzia wiki moja hadi mbili.

"Wengi wanaokuja hapa wanaotibiwa UTI, mtu anasema nimetibiwa UTI, nimepewa antibiotic nyingi, cha kwanza jiwe linapokuwapo pale, linavutia bakteria, hao bakteria watasababisha uharibifu.

"Kuna wengine wanakuja wanasema wanatokwa na damu kwenye njia ya mkojo, sasa pale ni kitu kingine, lakini likikaa sana, likaharibu seli zikawa zinaota kwenye mpangilio ambao siyo sahihi, inaweza kusababisha kansa," alisema.

Daktari bingwa huyo alitoa wito kwa Watanzania kujenga utamaduni wa kufanya vipimo vya afya mara kwa mara ili kupata matibabu.

Kaimu Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Dk. Kessy Shija, alisema madhara ya mawe ni pamoja na kuziba njia ya mkojo na ndani ya figo yanaharibu seli.

"Madhara yapo kama hayo na matokeo yake kile kiungo kinakufa kama hutofanya matibabu yake," alisema.

HABARI KITAIFA

# Bodi ya mikopo Zanzibar yachachamalia wadaiwa

**Na Mwandishi Wetu,**
PEMBA

BODI ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (BMEJZ), imesema imeshabuni njia nyingine ya kuwafuatilia wadaiwa, hasa ambao wameshaajiriwa na wamekaa kimya bila ya kuiarifu bodi.

Aidha, bodi imesema kuwa itahakikisha inamshughulikia mdaiwa mmoja mmoja.

Kauli hiyo ilitolewa na Mratibu wa bodi hiyo kisiwani Pemba, Ahmada Omar Juma, alipokuwa akijibu hoja za maofisa utumishi na wahasibu wa serikali kwenye mkutano wa kubuni mbinu ya urejeshaji wa mikopo ya bodi.

Alisema kuelekea mwaka 2020, bodi imeamua kufuatilia wadaiwa kwa utaratibu mwingine ikiwamo kwenda kwenye wizara moja moja na kumshughulikia mdaiwa mmoja mmoja, ambapo ziara hiyo, itaambatana na adhabu ya Sh. 50,000.

Alisema wapo ambao baada ya kumaliza masomo wameshaajiriwa zaidi ya mwaka mmoja, lakini hawajafika kwenye ofisi za bodi , ambako ndiko walikokopeshwa fedha.

"Tunaomba kuwaarifu tu kwamba, wale wote wanaoipiga chenga Bodi ya Mikopo, kwa kukaa kimya bila kutoa taarifa ya kuanza kukatwa mishahara yao sasa wajiandae... tutawafuata mmoja mmoja, na tukiwagundua wataandamwa adhabu faini ya Sh. 50,000,"alifafanua.

Katika hatua nyingine, aliwataka wanaokopa kuelewa kuwa fedha hizo sio ruzuku bali ni mkopo, unaohitajika kulipwa kwa wakati. "Ukikopa ujue kuwa kuna mdaiwa amesharejesha ndio maana na mwanafunzi mwingine akapata kukopa, sasa aliekopa akishindwa kurejesha anaukondesha mfuko wa Bodi," alieleza. Ofisa Mdhamini, wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba, Mohamed Nassor Salum, aliwataka maofisa hao kuvunja ukimya na kuweka kando udugu na ujamaa kwa watumishi wanaodaiwa na Bodi hiyo. Alisema serikali imeweka mazingira bora na rafiki kwa wanafunzi wa Zanzibar ili wasome bure kuanzia elimu ya maandalizi hadi sekondari, na kwa elimu ya juu imeweka mikopo yenye masharti nafuu zaidi.

"Nendeni popote mfuatilie aina ya mikopo inayotolewa, na kisha mfananishe na mkopo unaotolewa na wizara ya Elimu, basi mtaona huu wa kwetu, ni wa kiungwana zaidi,"alifafanua.

Baadhi ya washiriki wa mkutano huo, wameitaka Bodi hiyo kuongeza kasi ya kufuatilia wadaiwa kwa vile sheria inawaruhusu hadi kuwafungulia mashtaka. Mohamed Zubeir Ame, alisema lazima Bodi hiyo iweke pembeni urafiki na wafanye kazi kwa mujibu wa sheria ili wadaiwa wasidhani kuwa fedha hizo ni ruzuku.

Nae Tatu Abdalla Msellem, alisema wakati umefika kwa Bodi hiyo kuwatangaza wale wadaiwa sambamba na kuweka picha zao kwenye maeneo mbali mbali, inaweza kusaidia kufanya marejesho. Mohamed Kombo Juma, alisema wakati umefika kwa Bodi kuzihama ofisi zao na kuhamia kwenye taasisi na mashirika ili kuwatafuta wadaiwa wa bodi hiyo na kuanza makato.



Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee, akizungumza na vijana ambao ni wahitimu 54 wa mafunzo ya Mgambo (hawapo pichani) wilayani Masasi, mafunzo hayo yamefungwa jana katika uwanja Boma Masasi. **PICHA: HAMISI NASRI**

## Waziri abaini mazito malipo ya korosho

**Na Mathias Canal**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amefanya ziara ya siku moja wilayani Mkuranga Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, kukagua hatua zilizofikiwa za malipo ya wakulima wa korosho msimu wa mwaka 2018/2019.

Waziri Hasunga alibaini baadhi ya wakulima kutolipwa fedha zao jambo ambalo limemshangaza Kwa kuwa serikali ilishatoa fedha zote kwa ajili ya kuwalipa wakulima.

Alisema baada ya ziara ya kikazi katika mkoa wa Pwani, Lindi na Mtwara kubaini kadhia iliyopelekea kutolipwa fedha hizo serikali itachukua hatua za haraka.

"Sikutegemea hata siku moja kwamba eti itafika mpaka mwezi wa 12 wakulima wakiwa hawajalipwa kwa kuwa imetokea niwahakikishie wakulima wote ambao walileta korosho zao na zilipokelewa, wote watalipwa," alisisitiza Hasunga

Amesema wapo baadhi ya wakulima ambao wanasema hawajalipwa jambo ambalo sio kweli kwani wanafanya hivyo ili kukwepa madeni waliyokopa.

Kuhusu vibarua waliofanya kazi katika msimu huo wa korosho wa mwaka 2018/2019, Waziri Hasunga amesema kuwa madeni yote halali yatalipwa kwa wakati.

Hata hivyo ameeleza kuwa katika msimu wa mwaka 2019/2020, serikali haitajiingiza kwenye ununuzi wa zao la korosho badala yake imetoa fursa kwa wafanyabiashara kununua korosho.

Pia alisema kuwa serikali inaendelea kujipanga vyema ili katika siku za hivi karibuni isipange bei elekezi badala isalie kuwa msimamizi mkuu kuhakikisha haki inatendeka katika biashara hiyo.

# Brela yakuna wafanyabiashara usajili biashara kwa mtandao

**Na Mwandishi Wetu**,
MOROGORO

SIKU chache baada ya Serikali kupitia Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji, Angellah Kairuki kupongeza Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela) kwa kusajili majina ya biashara kwa njia ya mtandao, wajasiriamali mkoani Morogoro, wamepongeza hatua hiyo wakisema Brela imekomesha vitendo vya rushwa na ukiritimba.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana, walisema miongoni mwa vitu ambavyo wengi wamevutiwa navyo ni maendeleo ya teknolojia wakala huo umefikia kusajili majina kwa njia ya mtandao.

"Sasa hivi huhitaji kusafiri kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya kusajili jina la biashara kwani kupitia njia ya mtandao tumeweza kupata huduma ya usajili hali inayorahisisha utendaji kazi na imesaidia kupunguza gharama," alisema Hamza Kambaulaya, mfanyabiashara wa mitumba eneo la Mvomero.

Kambaulaya alisema vijana wengi wamepata mwamko wa kurasimisha biashara zao ikiwa ni pamoja na kusajili majina ya biashara hali inayowasaidia kuepuka kusumbuliwa na mamlaka mbalimbali za serikali na kuwafanya wawe huru katika shughuli zao.

"Mwaka mmoja nyuma nilikuwa nafanya biashara kienyeji hali iliyochangia kukosa uhakika wa maisha, lakini tangu nilivyorasimisha biashara yangu hali imekuwa tofauti na sasa wateja wengi wamekuwa na imani ni bisahara yangu," alisema Kambaulaya na kuongezea kuwa hali hiyo imehamasisha vijana kusajili biashara zao.

Alisema urasimishaji biashara ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za serikali ya awamu ya tano za kujenga uchumi wa kati na viwanda hivyo wataendelea kuhamasishana wenyewe ili kuwa sehemu ya kufanikisha azma hiyo.

Hashim Maulid, mfanyabiashara wa maji ya jumla katikati ya mji wa Morogoro, alipongeza mkutano wa mashauriano kati ya serikali, wawekezaji na wafanyabiashara ambao umekuwa chachu ya kuondoa kero na changamoto= za wafanyabiashara ili kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini lengo likiwa kukuza uchumi na kuondoakana na umaskini.

"Majadiliano yalikuwa ya uwazi kwa kila mmoja na kuwaleta baadhi ya mawaziri, manaibu waziri na wakuu wa taasisi na mamlaka mbalimbali kama uthibitisho tosha kuwa Serikali imedhamiria kuboresha mazingira ya kufanya biashara hapa nchini," alisema Maulid.

Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa Brela, .Loy Mhando,

Alisema wataendelea kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali kuhamasisha wafanyabiashara kurasimisha biashara zao ili kuwa sehemu ya kufanikisha azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

Mhando alisema Brela imejipanga kukomesha vitendo vyote vya rushwa, udanganyifu na ukiritimba ambao ulikuwa kikwazo kwa wafanyabiashara kusajili biashara zao.

# Waziri ahimiza nishati gesi asilia

**Na Mwandishi Wetu,** PWANI

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Musa Sima, ametoa wito kwa wawekezaji, wafanyabiashara na wananchi wote kuanza kutumia nishati ya gesi inayopatikana nchini hali itakayosaidia kupunguza uharibifu wa mazingira.

Akijibu hoja mbalimbali zilizoihusu ofisi katika mkutano wa majadiliano kati ya serikali, wawekezaji na wafanyabiashara mkoani Pwani kujadili changamoto zinazowakabali wafanyabiashara, Sima alisema wakati umefika kwa viwanda kujikita katika matumizi ya nishati ya gesi.

"Umefika wakati kwa wawekezaji hasa kwenye viwanda kuona haja ya kutumia nishati ya gesi asilia inayopatikana hapa nchini ili kupunguza ongezeko la hewa ukaa na pia kulinda mazingira," alisema Waziri Sima.

Alisema nishati hiyo inapatikana ni jukumu la wawekezaji na wafanyabiashara kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ili kujenga miundombinu ya kufika gesi hiyo katika maeneo husika ili ianze kutumia.

"Maendeleo ya ukuaji wa uchumi wa viwanda yatakuwa na maana kubwa kama kutakuwa na uzingatiaji wa kutunzaji mazingira ikiwa ni pamoja na matumizi ya nishati ya gesi ambayo ni rafiki kwa mazingira," alisema. Alisema serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara ili kuvutia wawekezaji ikiwa ni pamoja na utoaji wa vibali vinavyohusiana na uwekezaji kwa wakati ili kutokwamisha azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kazi na viwanda ifikapo 2025.

"Matumizi ya gesi asilia yatasaidia kupunguza ongezeko la hewa ukaa ambayo imekuwa tishio duniani kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia ya ongezeko la viwanda, hivyo kula kila sababu kama nchi kufanya jitihada za kuhamasisha matumizi ya gesi asilia," alisema Waziri Sima.

Alisema kupitia mikutano kama hii ya majadiliano inatoa fursa kutoa elimu na kuahamisisha matumizi ya gesi asilia na nishati nyingine mbadala kwa lengo la kulinda mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na baadaye.

"Matumizi ya gesi asilia ni madogo hapa nchini hasa katika viwanda kulinganisha na upatikanaji wake, hivyo nitoe wito kwa wawekezaji kutumia nishati ya gesi ili kuendelea kufanya uzalishaji hali itakayopelekea maendeleo nchini," alisema Naibu Waziri Sima aliendelea kusisitiza wawekezaji wa viwanda nchini kuwa na vitalu vya miti katika maeneo yao kama sehemu ya kuendelea kutunza mazingira na utekelezaji wa kanuni na Sheria ya Baraza la

Taifa la Hifadhi na Usimamzi wa Mazingira (NEMC) la kuwataka wenye viwanda kuwa na vitalu vya kuotesha miti.

Aidha, aliwapongeza wawekezaji na wafanyabiashara mkoani Pwani na maeneo mengine nchini kwa kuendelea kufata sheria na kanuni za nchi juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira na faidia zake.

Meneja wa NEMC Kanda ya Mashariki, Mhandisi Benjamin Mchwampaka, alisema baraza linaendelea kutoa elimu kwa wawekezaji na wafanyabiashara katika kuzingatia sheria za mazingira.

"Tayari wameshatembelea zaidi ya viwanda 300 mkoani Pwani kwa ajili ya kukagua utekelezaji wa sheria na kuwashauri juu ya utunzaji wa mazingira ikiwa ni pamoja na matumizi ya nishati mbadala kwa ajili ya uzalishaji," alisema Mhandisi Mchwampaka.

# Ujenzi madarasa wazuia vigogo likizo

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

ZAIDI ya wanafunzi 3,000 mkoani Iringa wamekosa nafasi za kujiunga na kidato cha kwanza mwakani, licha ya kufaulu mtihani kwa darasa la saba mwaka huu, huku vigogo wakinyimwa likizo kwa ajili ya kukamilisha ujenzi.

Hali hiyo imetokana na kukosekana kwa vyumba vya madarasa. Kutokana na hali hiyo, Mkoa wa Iringa umefanya kikao cha wadau wa elimu ili kutathmini na kujadili hali ya kielimu mkoani hapa, ambapo mwenyekiti wa kikao alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa Ally Hapi.

Wakati wa kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, alisimamisha likizo za wakuu wa wilaya, wakurugenzi, makatibu tawala wa wilaya na wa mkoa, maofisa elimu wilaya, wakuu wa idara ya elimu, maofisa mipango miji wa wilaya za Iringa na Kilolo mpaka hapo watakapokamilisha ujenzi wa madarasa kwa ajili ya wanafunzi watakaojiunga na kidato cha kwanza.

Hapi alisema hatarajii kuona wakuu hao wanaenda likizo wakati wanadaiwa ujenzi wa madarasa kwa ajili ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga elimu ya sekondari mwaka 2020 na kukosa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari.

Alisema jumla ya wanafunzi 22,130 walichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mkoani hapa, lakini kutokana na upungufu wa vyumba vya madarasa zaidi ya wanafunzi 3,480 watakosa kuanza elimu ya sekondari mwakani.

Hapi alizipongeza wilaya za Mufindi na Mafinga baada ya kufanikisha ujenzi wa madarasa na kupelekea wanafunzi wote 3505 waliofaulu darasa la saba kujiunga na sekondari mwakani.

"Sitarajii kuona wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri za wilaya, na maofisa elimu wanaomba likizo wakati wanajua baadhi ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza 2020 hawana mahali pa kwenda," alisisitiza Hapi.

Sera ya elimu na mafunzo ya ufundi ya mwaka 2014, imeelekeza kwamba kila mwananchi ana haki ya kupata elimu kadiri ya uwezo wake.

Kwa sababu hiyo serikali inachukuwa hatua za kuboresha, kuimarisha na kupanua wigo wa elimu kuanzia ngazi ya elimu ya awali hadi chuo kikuu. Hapi alisema ushirikiano unahitajika baina ya wananchi, serikali na wadau mbalimbali ili kuhakikisha kuwa elimu bora inapatikana kwa wote.

Baadhi ya wadau wa elimu walisema pamoja na elimu kutolewa bure, bado kuna changamoto hivyo ni vizuri serikali kwa kushirikiana na wadau wasaidiane kuangalia namna ya kupunguza au kumaliza kabisa changamto kwa elimu ya watoto.



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, akiwafundisha wakazi wa Kijiji cha Mtapenda wilayani Kaliua mbinu bora za kunyunyizia dawa za kuua wadudu waharibifu wa zao la pamba wakati akitoa elimu kwa wakazi wa Wilaya ya Kaliua jana. **PICHA: VINCENT TIGANYA**

# Wadau waombwa mchango kuleta tija utumishi wa umma

**Na James Mwanamyoto**

WADAU wa tija katika utumishi wa umma pamoja na wanazuoni wametakiwa kujadili na kuishauri serikali juu ya namna bora ya kuboresha utendaji kazi na kuongeza tija serikalini. Wito huo ulitolewa jijini Dodoma jana na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dk. Mary Mwanjelwa, wakati akifungua mkutano wa wadau kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, wenye lengo la kujadili uboreshaji wa utendaji kazi katika utumishi wa umma ili kuongeza tija.

Dk. Mwanjelwa amesema, mchango wa wadau hao utasaidia kuishauri serikali namna ya kuboresha utendaji kazi kwa watumishi wa umma na kuongeza tija ambayo itasaidia katika kutoa huduma bora kwa wananchi ambao ndio walengwa wa maendeleo na huduma zenye kiwango stahiki zinazotakiwa kutolewa na taasisi za umma.

"Nawasihi mjikite zaidi katika kuchambua na kutafakari kwa kina juu ya namna ya kuwa na misingi imara na vigezo vitakavyosaidia katika kuboresha zaidi utendaji kazi serikalini na kuongeza tija," alisisitiza Dk. Mwanjelwa.

Aidha, Dk. Mwanjelwa ameongeza kuwa, ongezeko la pato la taifa lolote duniani ndio msingi na chanzo cha kuboresha mishahara na masilahi ya watumishi, kuboresha maisha na kuwaletea maendeleo wananchi wake, hivyo wadau wanapaswa kuishauri vema Serikali kuongeza wigo wa mapato na hatimaye iweze kuboresha masilahi ya watumishi wa umma.

Mkutano huu wa siku mbili wa wadau wa kujadili uboreshaji wa utendaji kazi katika utumishi wa umma ili kuongeza tija umeratibiwa na Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kuiwezesha serikali kupata mchango na ushauri katika kuboresha utendaji kazi na tija ndani ya utumishi wa umma.

# Walioshindwa kuhudumia watoto kupelekwa kwa RC

**Na Allan Iack,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, amewaagiza wakuu wa wilaya kumpelekea takwimu halisi ya wazazi walioshindwa kutimiza wajibu wao wa kuwasomesha na kuwahudumia watoto wao.

Agizo hilo, alilitoa juzi wakati wa kilele cha Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia.

Pia amewataka wakuu wa wilaya mkoani humo, kutoa taarifa ya matukio ya ukatili wa kijinsia yaliyoripotiwa kwenye wilaya zao.

Alitaka katika taarifa zao, kuonyeshe hatua gani zilizochukuliwa, mashauri yaliyopelekwa mahakamani, na ambayo hayakupelekwa na vikwazo walivyokabiliana navyo.

Hata hivyo, amewataka wananchi kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi na wanasheria wanaoandaa mashtaka kwa ajili ya kupeleka shauri mahakamani.

"Kumekuwapo na tatizo kwa wananchi kutotoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi na wanasheria wanaoandaa mashtaka hivyo nawaomba wananchi wote tushirikiane kukabiliana na suala la ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake," alisema Gambo.

Pia alisema kikwazo kingine kimekuwa kwa watoa taarifa kuogopa kwenda mahakamani kutoa ushahidi.

"Naomba wananchi wenye nia ya kupambana na matukio haya kuwa tayari kutoa ushirikiano kwa mamlaka husika," alisema Gambo.

Aliagiza Jeshi la Polisi, dawati la jinsia kuwatafuta wazazi ambao hawatekelezi wajibu wao wa kusomesha watoto na kuwahudumia.

"Wapo watoto na mama zao wanaingia katika matatizo mbalimbali baada ya kukosa malezi kutoka kwa baba na waume zao," aliongeza Gambo. Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alisema jeshi hilo, limejipanga kuanzisha msako wa nyumba kwa nyumba kuwatafuta watu wanaojihusisha na ukatili wa kijinsia.

"Tumejipanga kupambana na wahalifu wanaojihusisha na ukatili wa kijinsia katika Mkoa wa Arusha," alisema Shana.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mkoa ya Mount Meru, Shafii Msechu, alisema hospitali hiyo, ina kituo maalumu cha kupokea waathirika wa ukatili wa kijinsia, kituo hicho kimefungulia mwezi Mei, mwaka huu. Alisema tangu kufungulia kwa kituo hicho, kimewapokea waathirika 333, na kesi zilizofikishwa mahakamani ni 19 zipo polisi kwa ajili ya upelelezi zaidi.

Katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ukatili wa Kijinsia, kitengo cha wanawake cha Jeshi la Polisi cha kupinga ukatili wa kijinsia kiliwatembelea waathirika katika Hospitali ya Mount Meru na kutoa msaada wa sabuni, khanga, maji ya kunywa na juisi kama ishara ya kupinga matukio hayo kwenye jamii.



Mfanyakazi wa usafi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha akizoa takataka bila ya vifaa vya kuzia mikono katika Mtaa wa Majengo jana. **PICHA WOINDE SHIZZA**

# Mhadhiri mbaroni madai ya kupokea rushwa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), mkoani Arusha, imemfikisha mahakamani jana Mhadhiri wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru, Abubakari Haliye, kwa madai ya kuwashawishi, kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa wanafunzi wa chuo hicho. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Takukuru kwa vyombo vya habari, mtuhumiwa akiwa katika utekelezaji wa majukumu yake ya ufundishaji aliwashawishi wanafunzi wa astashahada wa mwaka wa mwisho kumpa rushwa ya fedha ili kuwafaulisha katika mitihani yao ya marudio (suplimentary).

Taarifa ya Takukuru ilieleza kwamba uchunguzi walioufanya wamebaini mtuhumiwa huyo, aliwaomba wanafunzi hao kila mmoja kutoa, Sh. 50,000 ili awafaulishe mtihani.

"Ushawishi huo, aliufanya kwa kumtumia mwanafunzi ambaye jina lake limehifadhiwa kwa sababu za kiuchunguzi," ilidai taarifa hiyo.

Pia taarifa hiyo ilidai mwanafunzi huyo, alipokea fedha kutoka kwa wanafunzi wenzake na kuituma kwa mwalimu huyo, kwa muamala wa simu na benki. Mtuhumiwa huyo amefikishwa mahakamani jana, kwa tuhuma za kushawihi, kuomba na kupokea rushwa kinyume cha kifungu namba 15, cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

# Halmashauri kutekeleza miradi elimu, mazingira

**Na Daniel Sabuni,** LONGIDO

HALMASHAURI ya Wilaya ya Longido imetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za elimu, ujenzi na mazingira katika kipindi cha Julai hadi Septemba, mwaka huu na kutumia Sh. 17,608,813.

Peter Lekanet, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, alisema halmashauri ilikuwa na bakaa ya mwaka 2018-19 ambapo ilikisia kutumia 52,850,177 na hadi kufikia Septemba 2019, ilishatumia 17,608,813.

Alisema fedha hizo zilielekezwa kukamilishha ujenzi wa vyumba vya madarasa ya wasichana ya Sekondari ya Tingatinga, ukamilishaji wa jengo la ofisi za halmashauri, kukamilisha ufungaji wa mashine ya Mionzi (X-ray) katika Kituo cha Afya cha Longido.

Lekanet alisema kwa mwaka 2019/2020, halmashauri imepanga kutumia 505,450,000 kutoka mapato ya ndani, kutekeleza miradi ya maendeleo na hadi Septemba 2019, Sh. 97,923,225 zilishatumika kwa kuwezesha ukamilishaji ujenzi wa maabara tatu za shule za sekondari za Matale na kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Vile vile, alisema jumla ya doria 23 za kudhibiti uharibifu wa mazingira, misitu na uwindaji haramu wa wanyama pori katika maeneo mbalimbali ya wilaya zilifanyika na mtu mmoja alikamatwa kwa kuingiza ng'ombe 15 katika hifadhi ya mlima Longido na watuhumiwa wawili wa ujangili walikamatwa wakiwa na vielelezo vya nyara za serikali na wamefikishwa mahakamani.

Lekanet alisema hati 35 za umiliki wa ardhi zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa Kamishna Msaidizi wa Ardhi Kanda ya Kaskazini, zikiwamo hati nne za miradi na halmashauri imeshasaidia hati za kimila 40 katika maeneo mbalimbali ya vijiji vya halmashauri hiyo.

Alisema hati 74 zilitolewa kwa kampuni mbalimbali ya uwindaji wa kitalii yenye vitalu ndani ya wilaya. Hati hizo zimetolewa kwa kuzingatia Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009 na kanuni za uwindaji wa kitalii marejeo ya mwaka 2019.

Alisema michoro minne imeidhinishwa na Mkurugenzi wa miji na vijiji kwa ajili ya maeneo ya Oromba, Oltepesi na Ranch yenye jumala ya viwanja 2,600.

Diwani huyo alisema elimu ya ujasiriamali imetolewa katika kata ya Longido, Namanga, Engikareti, Olmolong na Tingatinga na jumla ya wanawake 1,589 na wanaume 712 walipatiwa mafunzo hayo hasa utengenezaji wa batiki, sabuni za maji, mafuta ya kupikia na uendeshaji wa biashara.

Alisema halmashauri pia imepokea maombi ya kampuni ya Land General Panning Company Limited na kuruhusiwa kufanya urasimishaji wa makazi holela katika maeneo ya wilaya kwa kushirikiana na wananchi na halmashauri.





# RAS achukizwa ubovu vyoo shuleni

**Na Godfrey Mushi,** HAI

TATIZO la ubovu wa vyoo katika Shule ya Msingi Mijongweni iliyopo Kata ya Mnadani, wilayani Hai, limemchefua Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro (RAS), Dk. Hatib Kazungu na kuagiza kila kaya kuachangishwa ili kumaliza tatizo hilo haraka.

Alitoa maelekezo hayo jana, baada ya kufika katika kata hiyo kuzungumza na wananchi na kujionea ubovu wa vyoo hivyo unavyotishia usalama wa watoto wanaosoma shuleni hapo.

"Mimi mwenyewe naanza kuchangia mifuko 20 ya saruji kwa ajili ya kuwaunga mkono wananchi kumaliza tatizo hili. Ndugu zangu hali kama hii ni hatari kwa afya ya watoto," alisema. "Siyo afya pekee, ukweli ni kuwa uhaba wa vyoo shuleni, unarudisha nyuma juhudi za walimu kutoa taaluma, kwa kuwa ni vigumu kwa mtoto kujifunza katika mazingira yasiyokuwa rafiki kiafya."

Kwa mujibu wa Dk. Kazungu, tatizo hilo kwa sasa limeota usugu katika shule za msingi kwa kuwa hali inaonyesha wazi kuwa shule nyingi za msingi hazina vyoo vinavyokidhi mahitaji ya wanafunzi.

Dk. Kazungu aliwataka wananchi wa kijiji hicho kuwa na tabia ya utayari kuchangia maendeleo yao kwa kuwa wanufaika wa miradi hiyo ni wananchi wenyewe.

Baadhi ya wananchi waliozungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti akiwamo Taretio Lukumay, alisema moja ya vyombo ambavyo vimepewa mamlaka ya kusimamia uendeshaji wa shule za msingi ni kamati za shule.

"Hiki ni kikundi cha wajumbe waliochaguliwa au kuteuliwa kwa kuzingatia nyadhifa zao ili kusimamia maendeleo ya shule za msingi kwa niaba ya jamii na ili kutatua tatizo la vyoo, tunashauri kamati zilizopo maeneo ya vijijini kutumia rasilimali zinazopatikana katika mazingira yao kama miti, mchanga, mawe na rasilimali watu," alisema Lukumay.

Mkazi mwingine wa kijiji hicho, Theresia Kasebo, alisema kinachohitajika ni namna ambavyo kamati hizo zitajipanga kuhamasisha jamii kushiriki kikamilifu kutatua tatizo la vyoo shuleni. Kuhusu kero ya barabara, Dk. Kazungu aliwahakikishia wananchi hao kuwa atashirikiana na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) ili kuhakikisha barabara zote zinazounganisha kijiji hicho na maeneo ya kutolea huduma muhimu zinapitika katika kipindi chote cha mwaka.



Machinga wakiwa katika Mtaa wa Kariakoo, Arusha wakisubiri wateja wa kununua miti ya Krismasi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# DC aamuru waliochota fedha Saccos kukamatwa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KAMATAKAMATA ya watu wanaodaiwa kuchukua mamilioni ya fedha za wanachama wa vyama vya akiba vya kuweka na kukopa (Saccos) kinyume na utaratibu wa vyama vya ushirika na kisha kukaidi amri ya kuzirejesha ndani ya siku 14 katika Wilaya ya Hai, imeanza rasmi.

Uamuzi wa kuwatia mbaroni wadaiwa hao ulitangazwa jana na Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai ole Sabaya, wakati akizungumza na wanachama wa Chama cha Akiba cha Kuweka na Kukopa cha Nshara Sacoss, kilichopo Machame.

Akiwa katika eneo hilo, Ole Sabaya aliagiza kukamatwa pia kwa Mwenyekiti mstaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Wilaya hiyo na kuhojiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Ole Sabaya alisema: "Kutozirejesha fedha hizo kwa muda mrefu ni kuzifanya hizi Saccos kuendelea kuwa hoi na kuwanyima wengine haki ya kukopa hata kama ni wanachama, kwa sababu wakubwa wamechukua fedha kinyume na utaratibu.

"Kwa hiyo hapa kwenye Saccos ya Nshara peke yake, wanachama wanadaiwa Sh. milioni 681 na Mwenyekiti wa Saccos aliyepewa heshima ya kulinda dhamana na fedha za watu unadaiwa Sh. milioni 13.5." Akiwa katika eneo hilo, Mkuu huyo wa wilaya alieleza kuwa watu wanaodaiwa kwenye vyama hivyo vilivyopo Wilaya ya Hai, ni jumla ya Sh. bilioni 1.45.

Kutokana na madai hayo, Ole Sabaya aliongeza: "Nimesema mimi sitamsubiri mheshimiwa Rais Dk. John Magufuli aje, halafu msimame hapa mseme mnadai halafu hakuna hata hatua inayochukuliwa, mheshimiwa Rais anakerwa na anaumizwa sana na anatamani vilio vya wananchi vikome, vifike mwisho."

Alisisitiza kuwa kama kuna mtu anazo hizo fedha za wanachama na alikuwa anataka kuacha kuzirejesha azilete kuanzia sasa, kwa kuwa amepanga atafanya ukamataji wa kihistoria kwenye wilaya hiyo.

Mkuu huyo wa wilaya alitangaza kuanza kwa operesheni ya ukamataji wa watu hao wanaodaiwa fedha hizo kuanzia jana. "Sina shida na mtu, nina shida na pesa za wananchi. Urudishe pesa hizo ili tukuambie nenda zako na usirudie kutenda tena dhambi hii au tukukamate kwa kosa la uhujumu uchumi kwa kutumia fedha za watu kinyume na utaratibu," alieleza Ole Sabaya.

"Kwa maelekezo hayo sasa, OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya), kamata watu wote hao sasa hivi, mkabidhi Takukuru, yaani hii ni operesheni inayoanza kuanzia leo wilaya nzima. Popote walipo waambieni wanachama wa Nshara Saccos, warudishe wenyewe vinginevyo tutawataabisha."

Pia Ole Sabaya aliagiza Jeshi la Polisi na Takukuru kuwasaka watu 11 walioshiriki katika ubadhirifu huo wa fedha hizo ambazo walizikopa tangu mwaka 2012 na kutoroka baada ya kusikia tangazo la kurejesha mikopo hiyo ndani ya siku 14 ambazo zimeisha jana.

# Adaiwa kujiua kwa kunywa maji ya betri

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WIVU wa mapenzi unadaiwa kusababisha mkazi mmoja wa Sanya Juu katika Wilaya ya Siha, Godlisten Godson (35), ambaye ni dereva wa basi dogo la abiria aina ya Noah kukatisha maisha yake kwa kunywa maji ya betri.

Mtu huyo anadaiwa kufariki dunia juzi, baada ya kufikishwa katika Hospitali ya Wilaya ya Siha akiwa hoi hajitambui.

Watu wa karibu na dereva huyo, wamelieleza Nipashe jana kuwa Godlisten alifariki dunia Desemba 10, mwaka huu, majira ya asubuhi, wakati anapatiwa matibabu hospitalini hapo.

Alipotafutwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP), Salum Hamdani, kuzungumzia taarifa za mtu huyo kudaiwa kujiua kwa kunywa maji ya betri, alisema mpaka sasa hana taarifa kuhusu tukio hilo na anafuatilia jambo hilo ili kufahamu ukweli wake.

Mmoja wa majirani wa dereva huyo, Merry Chacha, alisema kabla ya kuchukua uamuzi huo, kulikuwa na ugomvi wa muda mrefu kati ya Godlisten na mke wake.

"Hawa watu walikuwa na ugomvi wa mara kwa mara wa kimapenzi, mwanamke akimfuatilia mume wake akimhisi sio mwaminifu kwenye ndoa yao. Tunadhani labda kinaweza kuwa chanzo cha haya yaliyotokea na likamfanya mumewe akereke na kuchukua uamuzi huo mgumu," alieleza Chacha.

Alipoulizwa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Sanya Juu, Wema Gasino, kuhusu tukio hilo, alisema taarifa ya kukimbizwa kwa mtu huyo hospitali ya wilaya ili kuokoa maisha yake, alizipata juzi na jana asubuhi akajulishwa kuwa tayari amefariki dunia.

"Hili jambo ni la kuuzunisha kwa kijana kama huyo kuchukua hatua ya kukatisha uhai wake, tunapoteza nguvu kazi ya taifa kwa masuala ambayo yangeweza kumalizwa na familia zenyewe katika meza ya majadiliano," alieleza Gasino.

Alieleza kuwa hivi karibuni, kijiji hicho pia kilimzika mjomba wake na Godlisten kwa madai kama hayo ya kunywa maji ya betri.

Akisimulia tukio hilo, mke wa marehemu (jina limehifadhiwa), alisema jana asubuhi alikwenda kununua maziwa kwa ajili ya kupika chai na aliporudi nyumbani majirani wakamwambia mume wake amekunywa maji ya betri na amepelekwa hospitali ya wilaya.



Ukurasa 18

Kiuatilifu kipya 'kinachopromoti'mazao shamba, afya mlaji mbali na sumu kuvu



Ukurasa 19

DRC inatisha kwa ajali za ndege, ni kwa nini?



Ukurasa 14

## Vijana wafunguka udhaifu wao ulikojificha

# BUFE

Ijumaa Desemba 13, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



# Watalii 50 kutoka nchi 16 hifadhini Tunduru kwa mkutano kimataifa

## Mwanamuziki atumia nguvu sanaa kuwekeza kwao Afrika Magharibi

Ukurasa 20

## HISTORIA YAANDIKWA

# Watalii 50 kutoka nchi 16 hifadhini Tunduru kwa mkutano kimataifa

- Mara tu Hifadhi Mwambesi kuwa ya kimataifa
- Yumo Waziri Namibia, wa Afrika Kusini kibao
- Wazungu na majirani, wote wakiri 'kumenoga'

**Na Gideon Mwakanosya,** ALIYEKUWA TUNDURU

WATALII 50 Kutoka nchi 16 duniani, wameamua kufanya mkutano wao wa mwaka wa kimataifa katika Hifadhi ya Taifa ya Mazingira asilia ya Mwambesi iliyopo wilayani Tunduru, Mkoa wa Ruvuma.

Hiyo ni mara ya pili ndani ya kipindi cha miezi miwili kutoka mkoani Ruvuma, kupata makundi makubwa ya watalii kutoka nchi za Ulaya, Asia, Amerika na barani Afrika, inayofanya jumla ya makundi ya watalii 77 kutembelea hifadhi hiyo, iliyopandishwa hadhi kuwa ya kitaifa.

Msitu wa Hifadhi wa Taifa wa Mwambesi, ulianzishwa mwaka 1956 na ukapandishwa hadhi kuwa Msitu wa Taifa mwaka 2017/2018. Ni hadhi inayoongezeka kutokana na kuwa na utajiri wa viumbe vya kipekee duniani, wakiwamo wanyama, ndege na mimea.

Maximilian Jenes, Meneja Miradi wa asasi wakala ya Palms Foundation, anasema mkoa Ruvuma umepokea watalii 50 kutoka nchi 16 duniani waliopo nchini kwa namna mbili, watalii na wageni wanaoendesha mkutano wa kimataifa hifadhini Mwambesi.

"Mkutano huu wa kimataifa unahusiana na wadau viongozi wanaoongoza masuala ya uhifadhi duniani kutoka mataifa mbalimbali. Pia wamejadili na kuonyesha fursa mbalimbali zinazotokana na uhifadhi," anasema Jenes.

Meneja huyo anasema, ni mkutano unaolenga kuionyesha dunia fursa mbalimbali zinazotokana na uhifadhi na kwamba wananchi na wanajamii wanaozunguka hifadhi ya Mwambesi na Taifa kwa ujumla, wataweza kunufaika kupitia ziara za watalii wa namna hiyo.

Jenes anasema, mikutano ya namna hiyo imefanyika katika nchi mbalimbali za Afrika na nchini Tanzania ni mara ya pili. Kwa mara ya kwanza ulifanyika katika Hifadhi ya Taifa Serengeti, mkoani Mara. Hata hivyo hakutaja mwaka.

Anasema wakurugenzi wa Shirika la Palms Foundation ni miongoni mwa wanachama wa Umoja wa Mkutano wa Uhifadhi, hivyo waliweza kushawishi hadi kufanikiwa mkutano huo kimataifa kufanyika katika Hifadhi ya Taifa ya Mwambesi.

Katika ugeni huo, kuna Mtanzania na Waziri wa Biashara na Uwekezaji nchini Namibia, Leon Joste, huku Afrika Kusini ikiwa na wageni 16. Pia, wapo kutoka Ujerumani, Italia, Uingereza, Jamhuri ya Kidemokrasi Congo (DRC), Ufaransa, Finland, Ivory Coast, Australia, Gabon, Marekani na Uholanzi.



Wageni walipowasili katika Hifadhi ya Mwambesi. **PICHA ZOTE; GIDEON MAKANOSYA**

> **Mkutano huu wa kimataifa unahusiana na wadau viongozi wanaoongoza masuala ya uhifadhi duniani kutoka mataifa mbalimbali. Pia wamejadili na kuonyesha fursa mbalimbali zinazotokana na uhifadhi**

Anasema asasi yake kwa miaka mingi imekuwa inashirikiana na serikali katika uhifadhi na katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwamo Mkoa wa Ruvuma katika Hifadhi ya Mwambesi na upande wa Kaskazini, ni hifadhi za Tarangire na Manyara, ambako kazi yao inaendelea hadi sasa.

Jenesc anautaja Msitu wa Hifadhi ya Taifa ya Mwambesi, imehifadhiwa vizuri na ndiyo maana imekidhi vigezo vya kuwaleta wageni wa kimataifa, hata wakafanya mkutano wao wa siku tatu.

Anasema Palms Foundation kwa kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), wanatekeleza kwa vitendo sera ya Taifa ya kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo Kusini mwa Tanzania.

Waziri wa Biashara na Uwekezaji kutoka nchini Namibia, Leon Joste, aliyekuwamo katika ziara, ni miongoni mwa watalii waliofika katika hifadhi, anakiri kufarijika kuona hifadhi ya kipekee duniani ya Mwambesi yenye utajiri wa wanyamapori, mimea na ndege adimu ngazi ya dunia.

**MRATIBU UTALII**

Mratibu wa Utalii Kanda ya Kusini, ambaye pia ni Meneja wa Hifadhi ya Mwambesi, Deborah Emily, anasema ujio wa watalii 50 kutoka nchi mbalimbali duniani ni mwendelezo wa kupokea wageni na kuendelea kuitangaza hifadhi ya Mwambesi.

Anaieleza kwao ni faraja, kwa kwa sababu msitu huo sasa umepandishwa hadhi na katika mwaka 2018/2019 wamepokea watalii 77 kutoka nchi takriban 20 duniani, wakilenga kuona thamani ya uhifadhi wa mazingira asilia Mwambesi.

Anatoa rai kwa Watanzania kujenga mazoea kutembelea hifadhi, badala ya kusubiri

**INAENDELEA UK.15**



Moja kati ya ndege zilizowaleta watalii 50 katika Hifadhi ya Taifa ya



Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Jeremiah Sendoro (kushoto), akimsikiliza mmoja wa watalii katika Hifadhi ya Msitu Mwambesi.




Watalii walioweka kambi ndani ya fukwe za Mto Ruvuma, katika Hifadhi ya Taifa Mwambesi. **PICHA: MTANDAO.**

wageni kutoka nje ya nchi, akisisitiza hifadhi hiyo inafikika kwa urahisi kutoka Dar es Salaam. Ni umbali wa kilometa 890 kwa barabara.

Deborah anataja baadhi ya vivutio vilivyopo kuwa ni wanayama kama fukwe, mimea ya aina mbalimbali, Mto Ruvuma na ndege aina ya Pentiolem, ambaye dunia nzima anapatikana hifadhini Mwambesi pekee.



Mazingira asilia ya Mwambesi.

**WENYEJI WAZUNGUMZA**

Dismas Komba, Katibu Tarafa ya Lukumbule, ambayo Hifadhi ya Mwambesi inapatikana, anasema kupitia utalii wananchi watapata masoko na kuongeza pato la Taifa kupitia fedha za kigeni zinazotolewa na watalii.

Manyisye Mpokigwa ni Kaimu Meneja TFS, Kanda ya Kusini, anasema serikali kupitia watalii hao waliotembelea Hifadhi ya Mwambesi imeongeza fedha za kigeni hivyo kuchangia pato la Taifa kupitia sekta ya utalii.

"Mkoa wa Ruvuma haujawahi kupokea wageni wengi kutoka nchi 16 kwa wakati mmoja. hali hii inadhihirisha sasa milango ya utalii kusini inafunguka," anasema Mpokigwa.

Jeremiha Sendoro, Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, anasema amefanya mazungumzo na baadhi ya watalii na wamekiri kufurahia Hifadhi ya Taifa ya Mazingira Asilia Mwambesi, ambako wamekuwa wakisikia mingurumo ya wanyama, ndege na Mto Ruvuma.

Anaeleza kwamba, kutokana na Ruvuma kupata fursa ya wageni wengi kwa wakati mmoja, amewaomba wafike kufanya uwekezaji, kwa sababu mkoa unamaeneo mengi yanayofaa kuwekezwa katika nyanja mbalimbali ikiwamo uhifadhi, kutunza mazingira asilia, kilimo na kwenye viwanda na uvuvi.

Anasema uwekezaji utafungua ajira kwa vijana wengi ambao wanahitimu kila mwaka na kukosa ajira hivyo wanaweza kuajiriwa na kujiajiri.

Wilaya ya Tunduru inayopakana na mikoa ya Mtwara na Lindi, ilianza kufunguka kiuchumi zaidi, kuanzia baada ya mwaka 2006, Rais Jakaya Kikwete alipofungua miradi mikubwa ya barabara kati ya Msasi Mtwara na Tunduru na nyingine inayoiunganisha na Namtumbo, Ruvuma.

Ni hali iliyowezesha kuwapo mabasi mengi kutoka Dar es Salaam na mji huo, pia kutoka Masasi na mengine yanayopita katika mji huo kwenda mji wa Mbiga na Songea, ambako ni makao makuu ya mkoa.

- **Mwandishi anapatikana kwa mawasiliano simu:(+255) 0715928752 na baruapepe: gideonmwakanosya@yahoo.**

# Ndege ya Jeshi iliyotoweka Jumatatu imekutwa majini

**Santiago, Chile**

MABAKI ya ndege ya kijeshi ya Chile iliyotoweka siku ya Jumatatu wiki hii, yameonekana juzi.

Maofisa wa Jeshi la Chile, wanasema wamezuia mabaki yanayoaminika kutoka katika ndege hiyo ya kijeshi na yalipatikana yakielea umbali wa kilomita 30 kutoka eneo walilokuwa na mawasiliano ya mwisho.

Vifusi hivyo vilipatikana katika maji yanayojulikana kama mkondo wa Drake. Ndege hiyo ilikuwa inatoka katika mji wa Kusini mwa Chile - Punta Arenas, ikielekea kambi ya kijeshi ya Antarctica, alikokuwapo Rais Eduardo Frei Montalva.

Vifusi hivyo vinasadikiwa huenda vinatoka katika tangi la mafuta ya ndege hiyo, kwa mujibu wa Kamanda wa Wanahewa wa jeshi la nchi hiyo, Eduardo Mosqueira, alipozungumza na wanahabari juzi, kuhusu tukio hilo.

Anasema, Kikosi cha Wanahewa kinaendelea na uchunguzi kubaini kama kuna mabaki hayo ya uhakika ni ya ndege hiyo, iliyopoteza mawasiliano Jumatatu saa 12.00 jioni, muda mfupi baada ya kuruka kutoka mji wa Punta Arenas.

Kikosi cha Jeshi la Wanahewa, kilitoa ramani ya njia iliyofuatwa ndege na muda wake kwamba ilitarajia kutua saa moja na dakika 17 katika kambi hiyo ya Eduardo Frei Montalva.

Kazi ya kusaka angani na baharini ilianza muda mfupi baada ya ndege kutoweka na tayari mataifa ya Argentina, Brazil, Uingereza na Uruguay, yameshatuma ndege kusaidia utafutaji wa ndege katika maji hayo ya barafu, huku Marekani na Israel zikitoa picha za setelaiti.

Abiria wa ndege hiyo, watatu walikuwa wanajeshi wa Chile, kati yao wawili ni wenye vyeo vya Meja Jenerali na Luteni Kanali na raia wawili walioajiriwa na kampuni ya uhandisi na ujenzi Inproser.

Wa tatu askari ni mwanamke pekee, Claudio Manzo (37), aliyejiunga na wanahewa mwaka 2008 na alipendelea kusafiri kwa ndege kufanya uchunguzi ardhini, kwa lengo la kupata habari kutoka maeneo yalio mbali.

Walikuwa wanaelekea kufanya kazi katika kambi hiyo ya kijeshi. Pia, kulikuwapo mwanafunzi na abiria 15 wa wanahewa, akiwamo kijana Ignacio Parada (24), aliyetambuliwa kutoka chuoni kwake 'mwanafunzi bora.'

Alikuwa akisomea uhandisi katika Chuo Kikuu cha Magallanesna na katika safari hiyo alikuwa anaelekea katika kambi ya Antarctic kwa mafgunzo ya vitendo.

Pia, mfanyakazi wa kampuni ya Inproser, Leonel Cabrera na Jacob Pizarro, walikuwa wakielekea huko kufanya kazi katika kambi hiyo ya kijeshi.

- Soma makala zaidi ya ndege uk. 19



Picha ya ndege ya mizigo ya kijeshi muda mfupi kabla ya kutoweka. **PICHA: MTANDAO.**

## MAPINDUZI VIWANDA& KASI DIGITALI

# Vijana wafunguka udhaifu wao ulikojificha

- Walia simu zimewakamata kuliko
- Mabinti wafunguka iliko hatari yao
- Bosi TGNP: Mkae sawa, Tehama hiyo!
- Waziri: Tunaandaa, ulaji kazi kwenu



Mkurugenzi wa TGNP, Lilian Liundi.



Prof. Honest Ngowi, akizungumza. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Sabato Kasika**

ZAIDI ya vijana 100 kutoka mikoa mitano, wameshiriki kongamano liitwalo 'Ushiriki wa Vijana Kwenye Uongozi na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda" ikilenga kuwakuza katika uongozi na ushiriki wao kwenye shughuli za kiuchumi.

Vijana hao walitoka mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Morogoro, Mbeya na kukutana katika kongamano hilo lililofanyika Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wawakilishi wa kiserikali na wadau wa maendeleo.

Wengine waliohudhuria kongamano hilo wiki iliyopita, chini ya uratibu wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ni asasi za kiraia vituo vya maarifa, walimu na walezi wa klabu za jinsia.

Mchokoza mada katika kongamano, Profesa Honest Ngowi kutoka Chuo Kikuu Mzumbe, tawi la Dar es Salaam, anawataka vijana wabadilike na kwenda kidigitali.

Prof. Ngowi ambaye kitaaluma ni mchumi, anasema, shughuli za kiuchumi kuanzia kilimo na hata biashara, kwa sasa vinaendeshwa kidigitali, hivyo vijana hawana budi kufikiri mara mbili, ili washiriki kwenye uongozi na mapinduzi ya nne ya viwanda.

Msomi huyo anasema, katika dunia ya leo kuna uchumi wa kidigitali na kilimo cha kidigitali, vyote ni muhimu vijana wa Kitanzania wavielewe kwa ajili ya maendeleo yao.

"Tunachokiangalia kwa sasa kama waajiri ni ujuzi laini, ubunifu, uwezo wa kufanya kazi na wenzako na uwezo wa kutumia teknolojia ya kisasa. Hivyo, vijana fikirini mara mbili ili msiachwe nyuma," anasema Prof. Ngowi.

> **"TGNP tunatamani kongamano hili liwe chanzo cha taarifa kwa watunga sera kuwezesha kusikia mawazo ya vijana ambayo ni msingi katika uendelevu wa miradi yoyote ya vijana. Inabeba mawazo ya vijana wenyewe.**



Vijana wakifuatilia kongamano lao. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

Anafafanua kinachowakabili kimaisha ni kujiongeza kwa uthubutu na kujituma kwanza, wakiwa na wazo la biashara, badala ya kwenda kutafuta fedha za kukopa na kisha kufikiria biashara ya kufanya.

### WANENAVYO

Tabitha Elias anasema vijana wanajichelewesha wenyewe, wanashindwa na kubaki nyuma, huku mapinduzi ya nne ya viwanda yakiwapita kwa kasi kubwa.

"Ukitaka ujue kwamba vijana bado tupo nyuma huku mapinduzi ya nne ya viwanda yakiwa na kasi kubwa, angalia tu jinsi tunavyotumia simu zetu. Hii itakupa picha halisi ya jinsi gani tusivyoweza kunufaika na mapinduzi ya nne ya viwanda," anasema Tabitha.

Mwingine aliyejitambulisha kwa jina la Janeth John, anasema mapinduzi ya nne ya viwanda yana manufaa makubwa kwa wale ambao ni wepesi wa kung'amua mambo na kuziona fursa.

"Wanawake wamekuwa nyuma katika hili na ninafikiri wakati umefika wa sisi wanawake kuamka usingizini ili mapinduzi haya yasituache nyuma," anasema," Janneth.

Godfrey Thomas, anaeleza nafasi ya mchango wao mkubwa katika utatuzi wa changamoto zinazowazunguka, kwa vile wao ndiyo wanaozijua, hivyo hawana budi kuzikabili.

"Yaani ni kwamba, vijana wa Kiafrika tunapaswa kutengeneza majibu ya matatizo yetu wenyewe huku tukiongeza ubunifu," anasema Thomas.

Grace Mgumba anaanza na ukweli wa takwimu, vijana ni wengi kuliko wazee, pia katika kundi lao wa jinsia ya kike ni wengi zaidi, lakini wachache kwenye vyombo vya maamuzi.

"Bado wasichana hawajashiriki na hawajajua waitumie vipi teknologia ya Tehama (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kuchukua nafasi za uongozi," anasema Grace.

Wa mwisho ni Magdalena Gervas, anayesema: "Unapoona nguvu kubwa ya mabadiliko, ujue ni dalili kuwa unapaswa kushituka. Kama mwanamke, najivunia kuwa sehemu ya mabadiliko haya yanayotokea. Ni fursa kwetu tukiitazama kwa upana."

### LILIAN LIUNDI

Lilian Liundi, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP aliyeandaa kongamano, anasema,vijana ni kundi kubwa katika jamii na inapozugumzwa mapinduzi ya viwanda, ni lazima kuwazungumzia wao.

"Tunatambua kwamba Uchumi wa Viwanda Tanzania, umekuwa na taswira tofauti tangu tulipopata uhuru mwaka 1961, kutoka umiliki wa mkoloni na kumekuwapo mabadiliko makubwa," anasema Liundi.

Anafafanua kwamba, serikali inapoongelea Uchumi wa Viwanda, dunia ipo katika Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yanayotelekezwa sasa na kwamba, vijana wasipoelewa fursa zinazoambatana nayo, wataachwa na dunia, wabaki wakilaumu.

"Mapinduzi ya kwanza ya viwanda yalitoa fursa ya 'mechanization' nguvu ya mvuke na maji. Ya pili, uzalishaji kwa wingi viwandani kwa kutumia umeme; ya tatu yalikuwa ni mapinduzi ya kiektroniki; mifumo ya Tehama," anasema.

Lilian anafafanua mapinduzi ya nne yako hatua ya mbele zaidi katika kuendeleza uchumi wa kidigitali, kwamba maarifa ni muhimu kuliko vitu, matumizi ya roboti kwenye ufanyaji kazi, huku mitandao ikitumika zaidi.

"Mapinduzi haya yamebadili vitu vingi sana na pia jinsi tunavyoishi, tunavyofanya biashara na tunavyohusiana. Hivyo, kongamano litakuwa mahali sauti za vijana zitatoka na zitasikika," anasema.

Anaeleza, matumiani ya TGNP kuona vijana wanakuza uelewa wao, fursa na ushiriki kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda, kuhakikisha wa kike hawaachwi nyuma.

"Tunaamini katika kukuza uwezo wa vijana kwenye uongozi na ushiriki wao katika shughuli za kiuchumi, kwani hayo yakifanyika yanaweza kuimarisha uhusiano wa serikali na vijana," anasema.

Anatoa mfano wa uchaguzi na idadi ya kura kwenye nafasi mbalimbali za uamuzi, kwamba kuna haja ya kuwapo nia ya dhati ya kuongeza idadi ya vijana kwenye ngazi za uamuzi.

"Mara nyingi miradi ya vijana inaandaliwa bila ya ushirikishwaji kikamilifu wa mawazo yao. Hii inaminya ushiriki wao kwenye miradi hiyo," anasema na kuongeza:

"TGNP tunatamani kongamano hili liwe chanzo cha taarifa kwa watunga sera kuwezesha kusikia mawazo ya vijana ambayo ni msingi katika uendelevu wa miradi yoyote ya vijana. Inabeba mawazo ya vijana wenyewe."

Anafafanua kuwa, TGNP inatambua kila jambo linakuwa kidigitali inayoleta tofauti ya kibiashara na uongezaji thamani ya bidhaa, mawasiliano na mengine yenye taswira ya digitali, kama masoko kwa bidhaa zinazoandaliwa.

### NAIBU WAZIRI

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Josephat Kandege, ambaye pia alikuwa na ujumbe kwa vijana hao, aliwaambia kuwa, wajibu wa serikali ni kuweka mazingira rafiki ya kufanya kazi na vijana, ili watimize malengo yao, jambo linalofanyika.

"Ni lazima kushikana mikono na kusaidiana katika kufikia malengo, ambayo Watanzania kwa ujumla wao wameyapanga na suala hilo ni katika nyanja mbalimbali," anasema Kandege.

Anawataka vijana kutambuaa jambo la msingi ni kuunga mkono juhudi za serikali waweze kutimiza malengo waliojiwekea, kwa ajili ya maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

"Pia, ni vyema kutambua kufikia mwaka 2050, soko la ajira litahusisha zaidi weledi wa binadamu kuendesha utaalamu wa artificial intelligence (ubunifu wa juu)," anasema.

# Biashara katika picha



Wanachama wa kikundi kinachojishughulisha na kilimo cha Sweat no Sweet cha kijiji cha Bwasi, Musoma Vijijini mkoani Mara, wakivuna matikiti maji, katika shamba lao juzi, kwa ajili ya kupeleka sokoni. **PICHA: SABATO KASIKA.**




Mkurugenzi wa Airtel Money, Isack Nchunda, akizungumza wakati wa kuzindua kampeni maalum inayojulikana kama LIPA ADA kwa Airtel Money, itakayotoa suluhisho kwa wateja wa Airtel Money kufanya malipo yoyote ya karo za shule kwa kutumia akaunti zao za Aitel Money wakiwa popote katika kipindi hiki cha msimu wa Sikukuu na kuendelea. Kushoto ni Meneja wa Airtel, Jackson Mmbando na kulia ni Mkuu wa Kitengo cha lipa Ada kwa Airtel Money. Emmanuel Mwaisoloka




Mkurugenzi wa Biashara wa kampuni ya Sukari ya Kilombero (KSC),Fimbo Butallah, akiwaonyesha waandishi wa habari sukari ya chapa ya Bwana Sukari iliyofungwa kwenye pakiti za kilo tano, kwenye uzinduzi wa pakiti hizo uliofanyika jijini Dar es Salaam jana.Wengine ni Meneja Huduma za Wateja wa KSC, Matoha Dumea (kulia) na Ofisa Mauzo Lulu Ngimbwa. **PICHA: SABATO KASIKA**

BIASHARA

# Kiuatilifu kipya 'kinachopromoti'mazao shamba, afya mlaji mbali na sumu kuvu

- Hofu ya karanga, mahindi sasa basi
- Mifuko mipya kuhakikishia mazao

**Na Daniel Sabuni, Arusha.**

KUMEKUWAPO ongezeko la magonjwa ya saratani nchini na duniani, kutokana na sababu mbalimbali.

Imethibitishwa sasa, moja ya yanayochangiwa ni ulaji vyakula vilivyochafuliwa na sumukuvu, ikiwamo aina ya 'aflatoxin' ambayo teknolojia ya kibaiolojia ya kuidhibiti, imebaini kuwamo kwenye mazao kama nafaka ya mahindi na karanga.

Hiyo aina ya sumukuvu ambayo ni kemikali inayozalishwa na ukungu kwenye baadhi ya mazao ya chakula, hususan mahindi na karanga na ziko aina mbalimbali na zinapatikana kwa wingi katika nchi za ukanda wa tropiki, ikiwamo Tanzania.

Inatajwa hali ya hewa ya joto inachangia kuota fangasi katika mazao husika na yakiwa shambani, hata baada ya kuvunwa, wakati wa kusafirishwa na kuhifadhiwa.

'Aflatoxin' inazalisha madhara kwa kinga za mwili na kuathiri ukuaji wa watoto wakidumaa, ini inayokuwa na ongezeko la saratani, hata mhusika kupoteza maisha.

Katika jitihada za kuzuia madhara, kiwanda kimojawapo cha mjini hapa kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti na Kilimo (IITA), wametengeneza kiutailifu cha kibaiolojia.

**MTAALAMU MASOKO**

Mtaalamu wa Masoko wa mradi huo, Julius Nyabicha, anaeleza ni kiuatilifu cha kibailojia kinachotumika kwenye mashamba ya mahindi na karanga kupunguza madhara yake kiafya na kiuchumi.

Anasema, ni kinga inayoepusha sumu kuvu kwa asilimia 90, iwapo mkulima atazingatia kanuni bora za kilimo na utafiti wa kuangalia ufanisi wa kiutalifu uliofanyika katika maeneo mbalimbali nchini.

Hapo inatajwa mikoa ya Morogoro, Dodoma, Mtwara na Manyara, imeonyesha ufanisi.

Nyabicha anasema, kimsingi kiuatilifu hicho hakina madhara kwa afya ya udongo na binadamu na Kwamba, ni kinga ya kibaiolojia kudhibiti fangasi na inatumika shambani.

Anasema, kwa mahindi hutumika wastani wa wiki mbili kabla ya kutoa mbelewele na karanga hutumika wiki mbili kabla ya kutoa maua.

Kwa mujibu wa Nyabicha, ni kiuatilifu kinachopatakana kwa wakala wa pembejeo za kilimo nchi nzima, bei nafuu na utumiaji wake ni rahisi.

Anaongeza kwamba mkulima anatakiwa aandae shamba, kwa mbegu aliyoshauriwa na ofisa ugani wa eneo lake, apande kwa mpangilio inavyoshauriwa kitaalamu, apalilie kwa wakati, avune na kisha anaanike mazao kwa kutumia turubai, ili kuepuka kuchafuliwa na fangasi watokao katika udongo.

Nyabicha anasema, mazao yakianikwa kwenye udongo yanakuwa katika hatari ya kuchafuliwa kirahisi fangasi wanaotengeneza 'aflatoxin.'

Kwa mujibu wa meneja huyo, Tanzania sio nchi ya kwanza kuanza kutumia kiuatilifu cha kibaiolojia katika kudhibiti aflatoxin na anazitaja nyingine za Afrika ni Nigeria, Senegal na Gambia.

Tofauti kuu katika ulingo wa matumizi ni kwamba, ni sharti iwe katika eneo husika, huku akirejea mafanikio ya taifa la Nigeria imepata mafanikio makubwa kwenye udhibiti pamoja na kuzingatia kanuni bora za kilimo.

Takwimu nchini, zinaonyesha kuwa wakulima wa mahindi nchini hupoteza kwa wastani asilimia 30 ya mazao, kutokana na kushindwa kufahamu njia sahihi na salama za kuhifadhi mazao yao.

Anatoa mfano wa zao mahindi, kwamba yamekuwa yakihifadhiwa yakiwa na kiwango kikubwa cha unyevu kinachochochea uotaji fangasi, inayochangia kuharibu mazao.

Inaelezwa, iwapo mazao hayatatunzwa inavyostahili katika sehemu zinazoruhusu mashambulizi ya wadudu waharibifu, yanatengeneza mazingira wezeshi kuota fangasi.

Mazao yakishambuliwa, maana yake inashusha bei zake na ushambulizi unaopofika mbali, hata inaifikisha kiwango cha kukosa soko.

Pia, kuna mifuko ya kuhifadhia nafaka inayotengenezwa na wazalishaji viuatilifu hao, kuzuia hewa na unyevu kupita, jambo linalosaidia hifadhi ya nafaka dhidi ya mashambulizi ya wadudu, kwani hawawezi kuishi bila ya hewa.

Ni mifuko inayosaidia kuiweka salama na uwezo wa kutumika katika misimu mitatu ikirudiwa, mtazamo ni kuwalenga wadogo waliotapakaa nchini

Nyabicha anasema Tanzania imebahatika kuwa na ardhi kubwa yenye rutuba na mvua za kutosha, hali inayoifanya kupata mavuno mengi, ambayo sehemu kubwa inapotea kwa kukosa teknolojia ya kuhifadhi mavuno ya nafaka.

Ushauri wake ni kwamba, wadau wote wanaohusika na biashara ya nafaka wakihifadhi vizuri utasaidia kupatikana chakula cha ziada, hata ikauzwa katika soko la nchi jirani

Anaeleza kwamba, matumizi ya mifuko sasa yamefika katika soko la nchi 10 jirani, akitaja baadhi ni Ethiopia, Uganda na Kenya, zikiwa na faida nne ambazo ni

kukidhi mahitaji ya chakula, kuongeza kipato cha familia, mapato ya nchi na kulinda afya kiujumla.

Mazao makuu ya chakula yanayotajwa nchini ni mahindi, mtama, mpunga, ngano, maharage, muhogo na

viazi na jukumu la nchi katika sekta hiyo ni kutunza mazao ili kupata tija kwa pato la mtu mmoja na kitaifa kwa ujumla.




Mkulima kutoka Kiteto, akipokea maelekezo kutoka kwa ofisa mauzo, jinsi ya kutumia teknolojia za mifuko na aflasafe katika maonyesho mjini. **PICHA ZOTE: DANIEL SABUNI.**

> **"Kwa mujibu wa Nyabicha, ni kiuatilifu kinachopatakana kwa wakala wa pembejeo za kilimo nchi nzima, bei nafuu na utumiaji wake ni rahisi.**





Msimamizi wa masoko wa viuatilifu, Julius Nyabicha, akiwaelezea wataalam kutoka Wizara ya Kilimo, jinsi ya kuvitumia wakati wa Maonyesho ya Kitaifa ya Nanenane yaliyopita, mkoani, Simiyu.

BIASHARA

# DRC inatisha kwa ajali za ndege, ni kwa nini?

Na Mwandishi Wetu

- Tangu 1945 anga yake 'mwendo ajali'
- 2007; ajali nane kwa mwaka mmoja
- 1996; iliacha njia na kuua 237 sokoni




USAFIRI wa ndege unatajwa kuwa moja ya njia salama zaidi za usafiri duniani. Pia inaelezwa, katika baadhi ya mataifa yenye mifumo dhaifu ya usimamizi wa safari za ndege, pamoja na ukosefu wa miundo mbinu bora, inaweza kulihamisha hilo katika upande wa hatari.

Hapo ndipo inapotajwa usafiri wa anga, katika Jamhuri ya Kidemorasia ya Congo (DRC), ikirejewa ajali mbili za ndege zilizotokea hivi karibuni nchini humo, zimeibua maswali mengi kuhusu usalama wa usafiri wa anga.

Ya karibuni ni ajali iliyotokea kwa ndege kuanguka katika eneo la makazi jijini Goma, Mashariki mwa nchi hiyo na kuua watu 27.

Hapi ndipo penye msingi wa swali kwamba, DRC ni hatari kwa kiasi gani na taifa hilo likoje, ikilinganishwa na mengine duniani?

Takwimu kutoka kwa Aviation Safety Network, shirika linalofuatilia na kukusanya taarifa na maelezo kuhusu usalama wa safari za ndege, zinaonyesha DRC imekuwa na ajali nyingi zaidi za ndege za kubeba abiria barani Afrika, tangu mwaka 1945, wastani wa miaka 74 sasa.

Mtaaluma Dk. Daniel Kwasi Adjekum, kutoka Chuo Kikuu cha Dakota, Kaskazini mwa nchini Marekani, anasema kuwapo ajali nyingi za ndege DRC kunachangiwa na sababu kadha, ikiwamo ukubwa wa taifa hilo, mandhari ya nchi na mifumo dhaifu ya usimamizi wa safari za ndege.

Anasema kufanyika uchukuzi wa angani, ni jambo muhimu sana katika nchi hiyo, ikizingatiwa kwamba ndiyo njia pekee ya kutegemea kufika baadhi ya maeneo kitaifa na kimataifa.

Kati ya miji mikuu ya mikoa 25 nchini humo, ni miji minne pekee ambayo mtu unaweza kusafiri kwa uhakika kwa kutumia barabara kutoka mji mkuu Kinshasa.

**MAHITAJI YALIYOCHAKAA**

Pia, DRC ina miundombinu iliyochakaa katika viwanja vya ndege na mitambo ya kufuatilia na kuongoza safari za ndege. Sheria na mifumo ya kiufundi ya kusimamia uchukuzi wa angani, pia inatajwa kuwa na upungufu.

Taifa linatajwa kukabiliwa na changamoto za matumizi ya teknolojia zilizopitwa na wakati, pia matumizi ya ndege zilizoundwa miaka mingi iliyopita, ambazo si imara tena na mifumo yake si ya kisasa.

Tangu mwaka 2010, hadi sasa, The Aviation Safety Network, inasema kuna tatizo litokanalo na wahudumu na watumishi wa ndege, katika kukagua na kukarabati ndege na ufutiliaji wa nyendo za wanaozihudumia, kukikosekana kanuni sahihi za kufuata.

Pia, shirika linasema kuna baadhi ya ajali zinasababishwa na tatizo lisizoepukika, kama vile athari za kimazingira, mfano hai ni hali ya hewa, penye mvua kubwa na ukungu kuna wakati huathiri safari za ndege.

DRC iko katika ukanda wa tropiki inayokabiliwa na mvua kubwa za kila mara katika maeneo yake mengi.

**"Mtaaluma Dk. Daniel Kwasi Adjekum, kutoka Chuo Kikuu cha Dakota, Kaskazini mwa nchini Marekani, anasema kuwapo ajali nyingi za ndege DRC kunachangiwa na sababu kadha, ikiwamo ukubwa wa taifa hilo, mandhari ya nchi na mifumo dhaifu ya usimamizi wa safari za ndege.**

**KWINGINEKO**

Marekani ndiyo nchi inayoongoza duniani kwa kuwa na ajali nyingi zaidi za ndege tangu mwaka 2010, ikifuatwa na Russia, Canada, Mexico na Indonesia.

Pia, Marekani ndio nchi inayoongoza kwa kuwa na ndege nyingi zaidi zinazotapakaa katika anga yake, zikijenga mazingira ya kuwapo ajali nyingi.

Idadi ya watu waliokufa kutokana na ajali za ndege nchini Russia ni 532 tangu mwaka 2010, ikitajwa ni idadi kubwa zaidi ya vifo duniani, Indonesia ikifuatia kwa vifo vya watu 520 katika kipindi hicho.

Mataifa hayo mawili, kwa sasa yana idadi kubwa ya ndege zinazopaa na zinaendelea kuongezeka maradufu ndani ua kipindi cha muongo mmoja uliopita.

Wakati nchini Russia idadi ya wanaosafiri kwa kutumia ndege inatajwa kuongezeka mara tatu tangu mwaka 2009, huko Indonesia taifa likiloko katika mapinduzi makubwa ya kiuchumi, idadi hiyo imeongezeka mara nne.

Ikirejewa nchini DRC, idadi ya waliokufa kutoka na ajali za ndege takriban sawa na taifa la Nepal barani Asia taifa, ambalo pia lina mandhari magumu yenye milima mirefu.

Nepal ina changamoto kubwa katika kudhibiti safari za ndege kuhakikisha usalama wa usafiri angani na idadi ya watumiaji ndege imekuwa ikiongezeka maradufu.

MARUFUKU

Rekodi mbaya ya usalama wa usafiri wa ndege nchini DRC, imelifanya taifa hilo kuwa miongoni mwa nchi ambazo mashirika yake yote ya ndege hayaruhusiwi kuingiza ndege katika anga ya Umoja wa Ulaya (EU) au mashirika hayo yamewekewa vikwazo.

Lakini, kuna mataifa mengine 13 ya Afrika yenye rekodi ya shaka angani, Asia na Amerika Kusini.

Rekodi inayohesabiwa kuwa mbaya zaidi nchini DRC, ni ya mwaka 2007, kulipotokea ajali nane za ndege katika kipindi cha mwaka mmoja.

Pia, ajali mbaya zaidi ya ndege DRC ni ya mwaka 1996, pale ndege ya kusafirisha mizigo ilipoteza njia ilipojaribu kupaa na kuingia kwenye soko lililojaa watu na kuua watu 237.

- ***Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa za kimataifa***



Ajali za ndege nchini DRC katika picha tofauti . **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

## SARAFU MTANDAO...

# Mwanamuziki atumia nguvu sanaa kuweka kwao Afrika Magharibi

- 'Mji gulio' utakaonadi sarafu nyumbani
- Asili Senegal, maisha yake Marekani

**Na Nimi Mweta**

MWIMBAJI na rapa Akon, ambaye jina lake la kuzaliwa ni Aliaume Damala Badara Akon Thiam, anayeishi na kuimba nchini Marekani, mzaliwa wa Saint Louis, jimbo la Missouri Marekani mwaka 1973, sasa ameingia katika anga tofauti.

Wazazi wake ni raia wa Senegal na baada ya kuzaliwa akiwa na umri mdogo walirudi kwao na baadaye akiwa na umri wa miaka saba, walirejea tena Marekani.

Alisoma katika chuo kikuu cha Clark, huko Atlanta jimboni Georgia, ambacho kwa jadi kinahudhuriwa zaidi na wanafunzi wenye asili ya Afrika.

Taarifa zilizoanza kujitokeza mwisho wa mwezi Juni, zilisema kuwa Akon, kuna msanii mwingine mwenye sifa aliyeingia katika dimba la kuanzisha sarafu za mitandaoni, ambazo ni kama hisa zinazotegemea kuthaminiwa na watu tofauti kama ilivyo katika mnada.

Ni jitihada sehemu ya juhudi zake kurudisha alichopata katika maisha kwa jamii ya Senegal na kwingineko Afrika. Sarafu mtandao inayoitwa Akoin, inaelekea kuwa na uwezo wa kutoa mchango ambao si haba katika juhudi hizo, kwa mujibu wa alichosema, hata wachunguzi tofauti.

Mipango ya kuanzisha sarafu mtandao ilitangazwa katika tamasha la kimataifa la filamu linalofanyika kila mwaka huko Cannnes, kusini mwa Ufaransa, katika mandhari ambayo kwa miezi kadhaa hapakuwapo na maelezo ya kina kuhusu dhamira na mpangilio wake.

Haikuwa tukio la uzinduzi, lakini nia yake kutumia sarafu mtandao anayoianzisha kujenga kitu kama mji 'Akon Crypto City.' Kwa haraka ni mandhari ya kukaribisha vijana wabunifu, wawezeshwe kusonga mbele.

Kwa mujibu wa jarida linaloeleza yanayohusiana na sarafu mitandaoni, CoinDesk, 'Akon Cryto City' itakuwa asilimia 100 mji wa ki-sarafu wa Afrika kujikita katika sarafu hiyo ya mtandaoni.

Ni jaribio na ubunifu unaotokana na imani rapa huyo alishaeleza kuwa teknolojia anayoliita 'matofali-mnyororo' inaweza kuwa mwokozi Afrika kwa njia nyingi, kwani inarudisha uwezo wa watumiaji wenyewe kuamua.

### WADADISI

Kuna wadadisi wanahusisha sarafu mtandao, ni teknolojia inayorudisha nyuma usalama (wa thamani) katika mfumo mzima wa thamani. Ni hisia inayotokana na jinsi thamani za sarafu nyingi barani Afrika zinavyopotea kutokana na mifumo yao duni.

Matazamo ni kwamba, kutakuwapo sarafu mtandao katika mazingira ya sasa na hasa mpangilio utakaowekwa na washauri wake wajulikanao pia 'matofali mnyororo.'

Wananchi na hasa vijana, wanaweza kuitumia kwa njia zinazowawezesha kupiga kwa jambo wanalolifanya, tofauti na serikali zinapokuwa zinafanya maamuzi yote. Kwa kiasi kikubwa, kinawaangusha wahitaji na hasa vijana, wanaobaki kusota.

Ni wazo pana na la kushangaza, kwani hadi sasa sarafu mitandaoni imekuwa mseto wa soko la hisa na kamari, Ndio inazaa wazo la kuitumia kama mpangilio bunifu wa kuwezesha kukuza vipaji.

Kinachotakiwa sasa ni kuanzishwa biashara, huduma na hata bidhaa katika eneo maalum la kutumiwa sarafu aina hiyo, bila ya serikali kuanza kutia mguu.

Tayari mwimbaji huyo 'rapa' ameshatafuta na kupata eneo la ekari 200, litakalofanyiwa juhudi na Rais Macky Sall wa Senegal. Anachotazamia ni kujengwa jiji la 'Akon Crypto City.'

Kupitia ukurasa wake wa mtandao, ni mji wenye kutafsiri Waafrika kuokolewa kutoa 'dunia ya wazungu' na inatarajiwa kuwa wa kwanza duniani unaojikita katika sarafu mtandao au fedha sadikika, watu wakitazamia kupata faida kubwa kwa kushiriki ununuzi wa thamani zinazojijenga kama matofali.

Ni washiriki tu wanaopewa fursa na haki ya kukagua na kinachotokea na Akon ana uhakika thamani ya sarafu ya nchi yake kutoharibika, matazamio yakiwa kuongezeka thamani ya maisha kikawaida.

Kwa mujibu wa rapa huyo, nafasi yake inaishia katika kutoa wazo na mwendelezo na anawaachia wasomi wajenge.

Huko nyuma, mwaka 2014 msanii huyo, mtaalamu wa uwekezaji aliunda mradi aliyouita 'Kon Lighting Africa' ulilenga kuvuna nguvu za jua na kusambaza umeme kwa watu takriban milioni moja.

Ni mradi aliyoanzisha msanii huyo mtaalamu wa fani ya uwekezaji, akiwa na Thione Niang, mwenye asili ya Senegal, wote chimbuko lao eneo la Kaolack nchini Senegal, ambalo hakukuwapo huduma ya umeme.

Mwekezaji mwingine wa kimataifa kutoka Mali, kijana mwenzake, Samba Bathily alijiunga nao kwani amejikita katika fani ya umeme wa jua, akiendesha kampuni.

Hivyo Akon Lighting Africa ina washirika bora, wataalamu na waendeshaji waliokubuhu katika fani zao, na siyo mradi wa kutoa msaada kwa watu wengine kupata nafasi ya 'kupiga dili.'

Wachunguzi wa habari wanasema, vizuizi vya kibiashara ambavyo Marekani iliinua dhidi ya China, vimewasaidia kina Akon, kwani vimefanya kampuni za Kichina kurundika vifaa ambayo ni taabu kuvipatia sokoni.

Hivyo, vilifaa Akon Lighting Africa kupata nyenzo za taa barabarani na mifumo rahisi ya kufua umeme. Kampuni hiyo ikapata mkono kutoka China Jiangsu, shirika la ushirikiano wa kiuchumi na kiufundi, kupata vifaa vya 'sola' kutoka China.

### WAKWEPA MKOPO

Wachunguzi wanasema mchepuo huo wa kibiashara uliwawezesha kina Akon kukwepa kuomba mkopo kutoka ama Benki ya Dunia au Benki ya Maendeleo Afrika.

Alipohojiwa, Akon anasema mradi umefikia nyumba zaidi ya 5000 katika nchi 14 za Afrika Magharibi na hadi mwisho wa mwaka 2015 kupata umeme na badaa ya hapo, ni zaidi ya nyumba milioni moja.

Pia, kuna taa za barabarani 13,000 zimewekwa na waajiriwa wapatao 5,000 hadi mwisho wa 2015. Ni kwa msingi huo, uzoefu wa kufanya kazi katika mazingira ya kawaida na kusimamia gharama ambako Akon na marafiki zake wanaanza mradi wa 'mji sarafu.'



Mwanamuziki Aliaume Damala Badara Akon Thiam. **PICHA: MTANDAO**.

> "Haikuwa tukio la uzinduzi, lakini nia yake kutumia sarafu mtandao anayoianzisha kujenga kitu kama mji 'Akon Crypto City.' Kwa haraka ni mandhari ya kukaribisha vijana wabunifu, wawezeshwe kusonga mbele.





Baadhi ya wajasiriamali wa Jiji la Mbeya wakiendelea na biashara zao nje ya Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya eneo ambako wamekuwa wakizuiliwa kwa maelezo kuwa sio rasmi kwa kazi hiyo. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Watoto 4,300 waishi mazingira hatarishi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

ZAIDI ya watoto 4,300 wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, wamebainika kuwa wanaishi katika mazingira magumu kutokana na kulelewa na wazee ambao hawana uwezo hali inayowalazimisha kufanya kazi hatarishi kwa maisha yao.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya, Theresia Mwendapole, wakati wa mwendelezo wa maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia ambayo kimkoa yalifanyika katika uwanja wa Sinjili wilayani Chunya.

Alisema baadhi ya watoto hao wanalazimika kufanya kazi kwenye migodi na mashamba ya tumbaku ili wapate fedha za kujikumu kazi ambazo alionya kuwa ni hatarishi kwa maisha na umri wao mdogo.

Vilevile alisema watoto hao wanakabiliwa na hatari ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia ikiwamo kubakwa na kulawitiwa na watu wazima wanaamini ushirikina. Alisema baadhi ya watoto hao wamekuwa wakihudumiwa na Ofisi ya Ustawi wa Jamii ya Wilaya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na kwamba katika mwaka wa fedha 2018/2019 walihudumia watoto 326.

"Tulikuwa tunawahudumia kwa kuwapatia elimu ya ufundi, ya msingi na sekondari na baadhi tuliwaunganisha na familia zao, sasa ili tuandae taifa zuri ni lazima tushirikiane kuwalea watoto hawa bila kujali hali zao," alisema Theresia.

Aliwataka wadau mbalimbali mkoani humo kuwasaidia watoto hao wanaoishi katika mazingira hatarishi kwa kuwapatia chakula, mavazi pamoja na mahitaji muhimu kwa ajili ya shule.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi aliwatahadharisha wananchi wanaotelekeza watoto wao kuwa wanaweza wakakabiliwa na adhabu kubwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema kwa sasa serikali ya wilaya hiyo inashirikiana na baadhi ya wadau kuhakikisha utumikishwaji wa watoto kwenye mashamba ya tumbaku pamoja na kwenye migodi vinakomeshwa kwa ajili ya ustawi wa watoto hao.

Mahundi alisema watoto wote wenye umri wa kuwa shuleni wanatakiwa wapelekwe shuleni na kwamba kwa mzazi yeyote ambaye hatampeleka mtoto shuleni anaenda kinyume na sheria ya mtoto namba 21 ya mwaka 2009.

"Wazee wetu walitulea vizuri na ndiyo maana hata sisi tunaishi vizuri kwa hiyo na sisi ni wajibu wetu kuwalea watoto wetu katika mazingira ambayo yatawafanya waishi vizuri baadaye na waliendeleze taifa kikamilifu," alisema Mahundi.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo, aliwataka watu wenye uwezo kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalumu kwa ajili ya ustawi wao.

Aidha, alimpongeza mdau mmoja ambaye alimsaidia mtoto mwenye ulemavu kwa kumpa kitimwendo kwa ajili ya kumwezesha kwenda shuleni pamoja na kufanya shughuli zingine.

# Tari Uyole yaandaa mashamba maonyesho

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (Tari) kituo cha Uyole jijini Mbeya kwa kushirikiana na wadau wengine wa kilimo, imeanza maandalizi ya mashamba ya maonyesho ya kilimo biashara kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi na wakulima.

Mkurugenzi wa Tari Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, amewataka wakulima mkoani Mbeya na mikoa ya jirani kujitokeza kufuatilia kila hatua ya mashamba hayo ili waweze kunufaika na teknolojia bora za kilimo cha kisasa. Dokta Bucheyeki alitoa wito huo jana wakati akifungua kikao cha wadau wa kilimo kilichokutana kwa ajili ya maandalizi ya mashamba ya maonyesho ya kilimo biashara kilichofanyika katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Uyole jijini Mbeya.

"Katika kipindi hiki ambacho tunaanza maandalizi ya mashamba ya maonyesho ya kilimo biashara, tunatoa wito kwa wakulima kujitokeza kushiriki na kufuatilia kila hatua ya maandalizi ya mashamba hayo ili wajifunze teknolojia za kisasa za kilimo ambazo tutazitumia kuandaa mashamba hayo," alisema Dk. Bucheyeki. Alisema kuwa katika maandalizi ya mashamba hayo watatumia mbegu za kisasa, mbolea na viuatilifu vinavyokubalika kitaalamu hivyo ni fursa nzuri ambayo mkulima hapaswi kuikosa.

Baadhi ya wadau wa kilimo watakaoshiriki maandalizi ya mashamba hayo wamesema wamejiandaa vema kuandaa mashamba hayo kwa kutumia vifaa, mbinu na teknolojia za kisasa ili wakulima waweze kujifunza na kutumia mbinu hizo kuzalisha mazao mengi kwa tija.

Akizungumza kwenye kikao cha maandalizi ya mashamba hayo, mwakilishi wa kampuni ya uzalishaji wa Mbegu ya Meru Agro, Christopher Shimweta, alisema wamejiandaa kutumia maonyesho hayo ya kilimo biashara kuwaletea wakulima mbegu bora ambazo zitawasaidia kuzalisha mazao mengi na yaliyo bora. Alisema watayatumia maonyesho hayo kuwaelimisha wakulima aina mbalimbali za mbegu zinazofaa kutumika kwenye mashamba yao kulingana na hali ya hewa, aina ya udongo pamoja na namna bora ya kuzitumia ili waweze kupata tija kwenye kilimo chao.

"Tumejiandaa kutumia maonyesho ya kilimo biashara ya mwaka huu kuwaeletea wakulima mbegu zinazowafaa kwenye mashamba yao pamoja na kuwaelimisha namna ya kuzitumia ili waweze kuzalisha kwa ufanisi na wapate mazao mengi," alisema Shimweta. Mwakilishi wa kampuni ya kusambaza zana za kilimo ya Mashamba and Tractors Solution Ltd, Andrew Mahenge, alisema wakulima watakaojitokeza kushuhudia namna mashamba hayo ya maonyesho ya kilimo biashara yanavyoandaliwa, watanufaika kwa kuona zana za kisasa za kilimo zinavyofanya kazi na kuleta tija kwenye kilimo.

Alisema katika maonyesho hayo watatumia zana za kisasa, lakini rahisi zinazofaa kutumiwa na wakulima wadogo ambao kama watahamasika kuzitumia wanao uwezo wa kurahisisha kazi ya kilimo kwa kutumia muda mfupi mashambani, lakini kwa kulima eneo kubwa na kwa ufanisi.

## Wawekezaji wazawa wawekewa mazingira wezeshi Kusini

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

MENEJA wa Kituo cha Uwekezaji (TIC) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Venance Mashiba, amewahamasisha wawekezaji wa ndani kuweka vitega uchumi katika mikoa ya nyanda hizo, kwa kuwa ina fursa na maeneo yaliyoandaliwa.

Alisema kuna maeneo ya kutosha yaliyotengwa na kituo hicho yakiwamo ya viwanda na kwa ajili ya uwekezaji wenye tija.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja huyo alisema mikoa hiyo ina maeneo ya kutosha kwa ajili ya fursa za wawekezaji akitolea mfano kuwa kwa mkoa wa Mbeya pekee kuna maeneo mengi.

Alisema yapo ya viwanda vya kuchenjua dhahabu, kuchakata samaki, viwanda vya kusindika maziwa na matunda.

Alisema kupatikana kwa maeneo hayo kunatokana na jitihada za kituo cha uwekezaji kanda kuzihamasisha halmashauri kutenga na kuainisha sehemu zenye fursa za uwekezaji kwa ajili ya wawekezaji.

Akitoa mfano wa Mbeya pekee, Mashiba alisema Halmashauri ya Chunya kuna hekari 450 ambazo zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kuchenjua dhahabu, halmashauri ya Busokelo imetenga hekali 66.4 kwajili ya ujenzi wa viwanda vya kusindika matunda na maziwa.

Meneja huyo wa TIC alisema katika halmashauri ya Mbeya Jiji kuna hekari 74,169 kwa ajili ya viwanda vya aina mbalimbali.

Aidha, katika halmashauri ya Kyela zimetengwa hekari 99.5 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kuchakata samaki, kukoboa mpunga na kusindika mawese.

Pia alibainisha kuwa kwa halmashauri ya Mbeya zimetengwa hekari 3,805 kwa ajili ya ujenzi wa bandari kavu ambayo itarahisha usafirishaji wa mizigo katika maeneo mbalimbali ya ukanda huo wa kusini na nchi jirani.

Wilaya ya Mbarali alisema zipo hekari 37 zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na chuma na katika halmashauri ya Rungwe zipo 37 ambazo zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kusindika maziwa, matunda na ujenzi wa soko la kimataifa la ndizi.

Alisema TIC na Ofisi ya Mkoa wa Mbeya na mikoa mingine ya nyanda za juu kusini wanashirikiana kuwahamasisha wawekezaji ili waweze kuchangamkia fursa za uwekezaji kwa Mkoa wa Mbeya na mingine ya ukanda huo ili kufanikisha azma ya ujenzi wa viwanda.





# Huduma za kupunguza uzito kuwa rasmi wakati wowote

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa (BMH) imetangaza rasmi kutoa huduma ya upasuaji wa kupunguza uzito kwa watu wenye unene uliopitiliza, baada ya kupata mafanikio makubwa kwenye majaribio hayo.

Juni mwaka huu, hospitali hiyo ilifanya upasuaji kwa njia ya matundu kwa mteja moja jina tunalo mkazi wa Rukwa mwenye miaka 37, ambaye alikuwa na uzito wa kilo 120 na leo ana kilo 74.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Dk. Kessy Shija, alipozungumzia mafanikio ya BMH katika kipindi cha miaka minne serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli.

Alitoa maelezo hayo kwa timu ya maofisa habari wa wizara na taasisi za umma mkoani Dodoma. Alisema mgonjwa huyo alifanyiwa kwa majaribio na kumekuwa na mafanikio makubwa, hivyo wanatarajia kuandaa gharama ambazo watu wengi watazimudu.

"Tunajipanga ili kujua vitu vilivyotumika vina gharimu kiasi gani, tukijua gharama halisi tutawatangazia," alisema.

Akizungumzia mafanikio hayo, Dk. Shija alisema hospitali ina vifaa tiba vya kisasa vinavyotumia teknolojia ya hali ya juu ikiwamo CT-Scan, MRI, na maabara ya kisasa ya uchunguzi na matibabu ya moyo.

"Huduma hii ya maabara ilianza Februari 2019, jumla ya wagonjwa 41 walihudumiwa hadi kufikia Juni 2019," alisema.


Alieleza kuwa hospitali imepunguza rufani za wagonjwa kwenda nje na hadi Juni 2019, wagonjwa saba walipandikizwa figo.

"Wiki ya kwanza ya Januari mwaka 2020 tunatarajia kupandikiza wagonjwa sita figo na taratibu zote za upandikizaji hao zimekamilika," alisema.

Aidha, hospitali imeendelea kutoa huduma ya ufuatiliaji kwa wagonjwa waliopandikizwa figo hadi Juni kulikuwa na wagonjwa 15, kati yao saba walipandikizwa BMH, sita nchini India na wengine wawaili Muhimbili na Uingereza. Kadhalika, alisema hospitali hiyo ilianzisha huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo zisizofanya kazi na mpaka sasa wamehudumia mara 2,974 kwa wagonjwa 86.

Kwa upande wa matibabu ya saratani, mkurugenzi huyo alisema hospitali imeanzisha huduma ya matibabu hayo na wagonjwa wanapata tiba.

"Pia kwa kushirikiana na serikali ya Israel imeweza kuanzisha huduma za matubabu ya dharura kwa majeruhi wa ajali mbalimbali, na pia tuna jengo la kisasa la kuhifadhia maiti ambalo lina uwezo wa kuhifadhi miili 36 kwa siku," alisema.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (watatu katikati), akipokea mfano wa hundi ya Sh. milioni 200 ikiwa ni gawio serikalini kutoka Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI), kushoto ni Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Patrick Ngwediagi, makabidhiano hayo yalifanyika jana jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mrundikano madarasani kikwazo ubora wa elimu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MRUNDIKANO wa wanafunzi madarasani umetajwa kuwa moja ya changamoto katika sekta ya elimu, hali inahitaji serikali kuchukua hatua za haraka kuboresha ufundishaji ili kupate elimu bora.

Hayo yalibainishwa jana na Mratibu wa mtandao wa elimu Tanzania (TenMet) Ochola Wayoga, wakati akifungua mkutano wa 11, wa mwaka wa mtandao huo uliojumuisha wadau mbalimbali wa elimu.

Wayonga, alisema kutokana na jitihada za serikali kuja na dhana ya elimu bila malipo uandikishaji wanafunzi nchini umeongezeka kwa kasi kubwa, hali inayosababisha ongezeko la wanafunzi katika shule nyingi.

"Kuongeza uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza ni jambo zuri sana kwani ni sehemu ya kuboresha elimu lakini sasa kinachotakiwa kufanyika kwa haraka ni kuboresha miundombinu kwani idadi ni kubwa, lakini miundombinu ni ile ile," alisema Wayoga.

Alifafanua kuwa hivi sasa kutokana na ongezeko la udahili wa wanafunzi wa darasa la kwanza pamekuwapo na marundikano wa wanafunzi katika vyumba vya madarasa, lakini uwiano wa kati ya walimu na wanafunzi bado haulingani kabisa.

"Changamoto nyingine katika elimu yetu kwa sasa ni uhaba wa madawati, matundu ya vyoo, vyumba kwa ajili ya watoto wa kike kujistiri wakati wa hedhi, lakini vifaa vya kufundishia na kujifunzia havitoshi kuna sehemu wanafunzi sita wanachangia kitabu kimoja wakati inatakiwa kila mmoja darasani na kitabu chake," alisema.

Alisema katika mkutano huo pia watajadiliana kwa pamoja ubora wa elimu nchini kwa kipindi kilichopita na kijacho ili kuona nini kinaweza kuwa suluhisho la kuongeza ubora katika sekta hiyo nchini.

Meneja Programu wa Mtandao wa Elimu TenMet, Nicodemas Shauri, alisema katika kipidi cha nyuma walikuwa wakipigania serikali kuongeza uandikishaji wanafunzi wa darasa la kwanza lakini sasa kuna haja ya kuangalia elimu wanayoipata kama ina ubora.

"Lazima tuangalie elimu wanayoipata vijana wetu mara baada ya kumaliza inaweza kuwasaidia vipi katika kuendesha maisha yao. Tumekuwa tukisikia kuwa vijana wetu hata wale wa chuo kikuu wanaomaliza wanashindwa kuajirika maeneo mbalimbali," alisema Shauri.

Alieleza kuwa ni lazima kama taifa kuangalia wanafunzi wanasoma kwa ajili ya nini ili kusaidia kuwaanda vijana na watakapo maliza elimu yao wawe na uwezo wa kuajirika au kujiajiri wenyewe katika eneo walilosomea.

"Lakini pia inabidi tuangalie katika suala la ufaulu ambao hivi sasa unaonekana umependa lakini tunaambiwa kule Ukerewe kuna wanafunzi wengi wamefaulu lakini hawajui kusoma wala kuandika," alisema Shauri.

Ofisa Programu wa Shirika la Sense International Tanzania, Benjamin Kihwele, alisema serikali inatakiwa kuweka katika sera ya elimu kipengele cha wasaidizi wa walimu katika elimu jumuishi ili kuwasaidia watoto wenye ulemavu mbalimbali kama kutokusikia upofu.

## Naibu Waziri awavaa wanaoibeza elimu nchini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, William ole Nasha, amesema pamoja na changamoto nyingi zilizopo nchini katika elimu, wanafunzi wana uwezo wa kutoa ushindani katika sekta ya elimu kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na zile za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Ole Nasha aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya kuwatunuku vyeti washindi wa kitaifa wa shindano la uandishi wa insha za SADC na EAC.

Naibu Waziri huyo alisema pamekuwapo na maneno ambayo yakiendelea kuwa elimu ya Tanzania haina ubora kumbe hali ni tofauti kwani vijana wamekuwa wakitoa ushindani kutoka katika jumuiya hizo. "Nawapongeza sana washindi wa shindano hili kwa sababu wamewadhihirishia kuwa elimu yetu ni bora," alisema Naibu Waziri.

Alisema huwezi kusema leo hii elimu yetu haina ubora wakati vijana wametoa ushindani katika mashindano ya uandishi wa insha kwa wenzao wa SADC na EAC.

Kutokana na hali hiyo aliwaagiza wakuu wa shule kuendelea kuwashawishi wanafunzi kuchangamkia fursa za mashindano kwani yanawasaidia kuongezea uwezo wa wao katika kukuza ujuzi wa lugha na maarifa kwa ujumla.

Alisema mashindano hayo yatawapa uwelewa mbalimbali wa mada za masomo mengine ambayo yatawajenga wanafunzi siku za usoni kunufaika na mtangamano wa Jumuiya hizo katika kujipima kujilinganisha na nchi nyingine. Mbali na hilo aliwataka wanafunzi walioshinda katika mashindano hayo kuwa kichocheo kwa wengine ikiwamo kutoa hamasa ili na wengine washiriki katika mashindano ya uandishi wa insha.

Wanafunzi 12 wa Tanzania walitunukiwa vyeti kutoka sekondari za Longido, Kibasila , Heritage Pwani, St Maxmillian Mbagala Sekondari.

Sekondari ya Kibaha Pwani, Tanga Tech, Loyola , Ben-Bella Sekondari ya Mjini Magharibi Waliopata tuzo za SADC in kutoka Longido, Morogoro na Kilangalanga Sekondari iliyoko mkoani Pwani.

Mratibu wa mashindano hayo, Sylivia Chinguwile, alisema mchakato wa kupatikana washindi huanza baada ya kikao cha wakuu wa nchi wanachama kutoa azimio.

Alisema baada ya hapo kila nchi mwanachama huwajibika kutangaza na kubainisha vigezo vya ushiriki kama ilivyoelekezwa na sekretarieti.

"Insha huwasilishwa wizarani baada ya kuchujwa katika ngazi ya shule na kusahihishwa na jopo la wataalamu," alisema Chinguwile.



## Vita dhidi ya ukatili kuendelea kupiganiwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JAMII imetakiwa kupiga vita dhidi ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia ambao unaonekana kuongezeka siku hadi siku.

Msaidizi Mkurugenzi wa Huduma za Kinga na Elimu ya Afya wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja, Dk. Himid Juma Said, alitoa rai hiyo katika maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia na Watoto yaliyoandaliwa na mradi wa jinsia na uhusiano wa imani, hafla iliyofanyika Nungwi Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema ni vyema wananchi wakashirikiana kulipinga janga hilo ili lisiendelee kuwaathiri wanawake na watoto.

Pia alisema serikali kupitia wilaya hiyo ipo imara kuhakikisha vitendo hivyo vinapungua na hatimaye kumalizwa ili visiendelee kuathiri nguvu kazi ya taifa.

Naye Mratibu wa mradi wa jinsia na uhusiano wa Imani, Niwaeli Justine, alisema wamefanikiwa kutoa elimu ya kupambana na ukatili wa kijinsia na kushajihisha suala la amani kupitia sehemu mbalimbali wakiwa na lengo la kufikia usawa wa kijinsia na kukuza ushirikiano wa amani na utulivu nchini Tanzania.

Alisema hadi sasa wamefanikiwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanafunzi na walimu zaidi ya 1150 kutoka dini ya kiislamu na ya kikristo.

"Mpaka sasa mradi huu umenufaisha watu wa jamii ya Zanzibar yani Unguja na Pemba zaidi ya 1,150 kati yao wanawake ni 695 na wanaume ni 455, Wakristo ni 366 na Waislamu 784," alisema.

Aliiomba serikali kuwapa ushirikiano wao katika kutoa mafunzo ili jamii iweze kuhamasika zaidi kuhusu kupinga ukatili wa kijinsia.

Kwa upande wake mwalimu kutoka taasisi ya dini ya Kiislamu ya Labbaika, Idrisa Hoja Haji, alisema suala la unyanyasaji wa kijinsia linapaswa kukemewa kwa nguvu zote kwa kuwa linarejesha nyuma maendeleo ya watoto na kuwapotezea ndoto zao.

Naye Mchungaji kutoka Kanisa la KKKT, Lidya Mwimi, alitaka jamii kuacha kuwanyanyasa watoto na badala yake kuwasaidia kupata haki zao za msingi ikiwamo kupata elimu.

# Yatakiwa mafunzo lugha za alama

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya Zanzibar, Asha Ali Abdalla, amesema utekelezaji wa mafunzo ya lugha ya alama ni jambo muhimu ambalo litasaidia kuondoa changamoto zinazowakabili wananchi wenye mahitaji maalum kufahamiana kwa urahisi wanapotaka kupatiwa huduma mbalimbali.

Akifungua mafunzo mjini Zanzibar ya lugha ya alama kwa watendaji wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar, alisema kuwa mafunzo hayo ni muhimu kwa taasisi zote ambazo zinatoa huduma kwa wananchi ili kujenga uelewa kwa wananchi wenye mahitaji maalumu.

"Sera ya Afya tutoe huduma ya afya bila ya ubaguzi kwa watu wote hata kama wana mahitaji maalumu ya viungo, akili, wasioona, viziwi na wenye maradhi ya ngozi wote wana haki sawa katika kupata huduma," alisema Katibu huyo.

Aliwataka wenye kutoa huduma pamoja na jamii kubadilike kwa kujua tofauti zilizopo baina yao na kuhakikisha wanapatiwa huduma kwa kuzingatia wao hawako katika mfumo wa kawaida kutokana na upungufu walionao.

Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa, Zahran Ali Hamad, aliwataka wafanyakazi hao kuwa makini kujifunza na kujenga uelewa wa kuimarisha mawasiliano wakati wanapotoa huduma kwa wananchi hao ili kuwaondolea changamoto wanazokumbana nazo. Vile vile, alisema ni jambo la kusikitisha kuona watoaji wa huduma za afya ikiwamo madaktari kutoelewana na mgonjwa mwenye mahitaji maalumu jambo linalochangia unyanyasaji na kuhisiwa wanapoteza muda kwa kutofahamiana kwao.

Alisema jambo hilo linachangia kupata unyonge kwa kushindwa kujielezea na kutolewa ukali, kukosa uelewa wa matumizi ya dawa wanazopewa pia kukaa foleni kwa muda mrefu kutokana na kutosikia wakati wakiitwa kupatiwa huduma.

Kwa upande wa Mkurugenzi Uendeshaji na Utumishi Wizara ya Afya, Ramadhan Khamis, alisema uanzishwaji wa mafunzo hayo muhimu kwa watoa huduma utasaidia kuonyesha njia kwa taasisi mbalimbali kujifunza ili kusaidia watu wenye mahitaji maalum.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Viziwi Zanzibar (CHAVIZA), Asha Ali, alisema amefurahishwa kwa juhudi ya Wizara ya Afya kuanzisha mafunzo ya alama za vidole kwa watendaji wake ili kuweza kuwarahisishia mawasiliano wanapohitaji huduma.



Katibu Mkuu Wizara ya Afya Asha Ali Abdulla akizungumza katika uzinduzi wa Mafunzo ya Lugha ya alama kwa wafanyakazi wa Bohari kuu ya dawa katika Ukumbi wa Bohari kuu ya Dawa Maruhubi Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ataka ufuatiliaji umiliki ardhi uwanja wa ndege

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Dk. Sira Ubwa Mamboya, ameutaka uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kuendelea kufuatilia umiliki wa ardhi wanapotarajia kujenga uwanja wa kutua chopa katika kijiji cha Paje, Mkoa wa Kusini Unguja.

Akizungumza wakati akikagua eneo hilo alisema, kupatikana kwa umiliki wa adhi hiyo kutasaidia kuondokana na usumbufu kwa wananchi wakati wa ujenzi.

Alisema kwa sasa kama hakuna kikwazo na wananchi wameshalipwa ambao walikuwa wamiliki ardhi hiyo waendelee na utaratibu ulioanza kufanywa.

"Ni jambo jema kuona mambo yote yapo sawa kwa wananchi na imani yangu ujenzi utaendelea vizuri ila tuharakishe umiliki tumeupata ili tukijenga tuwe na uhakika wa kumiliki eneo hili," alisema.

Naye Ofisa Miradi kutoka Mamlaka hiyo, Hafsa Ali Mbaruk, alisema kuwa eneo hilo lina ukubwa wa mita 200, na ujenzi huo umekuja kutokana na kukua kwa sekta ya usafiri wa anga pamoja na sekta ya utalii, mamlaka imeona ipo haja ya kujenga kiwanja ambacho kitaweza kutua chopa ili kurahisisha usafiri.

Alisema uwanja huo utawanufaisha watalii na wananchi ambao watakuwa wanatumia usafiri wa anga kwa njia ya helikopta kutoka Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume hadi uwanja wa Paje.

"Hii pia inatokana na imani wa wamiliki wa hoteli zilizopo ukanda huu kwa kuwa wanadai kuwa masafa ni makubwa ya barabara kutoka mjini hadi katika hoteli zao," alisema.

Alisema lengo kuu la mradi ni kuweka uwanja mbadala wa uwanja uliokuwapo kutumi katika njia ya uokozi kwa ndege, inayopata dharura pamoja na kukuza katika sekta ya utalii.

Alieleza kuwa kwa sasa wameshafanya dizaini ya michoro pamoja na sehemu ya baraza na wameshapata wataalamu kwa kuangalia na kupatiwa makisio ya barabara.

Alisema kwa kuanzia wataanza na ujenzi wa kilomita moja na upana na mita 80 na aina ya ndege zinazotarajiwa kutumia uwanja huo ni za karavani ambazo zitakuwa zinachukua abiria 13.

Kwa upande wake, Muhandisi wa Mamlaka hiyo, Khamis Muhidini Bakari, alisema, maandalizi ya uwanja yameshakamilika na tathmini imeshafanyika kwa wananchi waliopo katika eneo hilo.

Alisema kwa sasa eneo hilo limeshasafishwa na wameshaweka alama ya mchoro wa uwanja huo, utaanzia na jengo la muda na baadaye litakuwa la kudumu na litakuwa na sehemu ya maegesho.

# 'Korosho kichocheo kuvunjika ndoa'

**Na Hamisi Nasiri,**
NANYUMBU

MALIPO ya korosho kwa wakulima wilayani Nanyumbu mkoani Mtwara yametajwa kuwa chanzo kikuu cha kuvunjika ndoa na uwapo wa vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia.

Kutokana na hali hiyo, zaidi ya familia 50 wilayani humo zimetelekezwa ndani ya miezi mitatu iliyopita.

Aidha, imeelezwa kuwa fedha za korosho zimekuwa zikiwachanganya hasa wanaume ambapo wanapopata malipo yao kuamua kuvunja ndoa zao na kuoa wanawake wengine kwa kisingizio cha kuwa na fedha nyingi za korosho.

Hayo yalisemwa wilayani Nanyumbu na Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Nanyumbu, Fanuel Machumu, wakati wa kilele cha Siku 16 za Kupinga Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia, sherehe hizo zilifanyika mjini Mangaka wilayani Nanyumbu.

Machumu alisema licha ya familia zaidi ya 50 kutelekezwa pia katika kipindi hicho cha miezi mitatu iliyopita, zaidi ya watoto 10 hadi 15 wamepata ujauzito na kukatishwa masomo. Alisema matatizo ya mimba kwa watoto wakiwamo wanafunzi ni vitendo ambavyo katika Wilaya ya Nanyumbu bado vimeendelea kuonekana ni jambo la kawaida kwa jamii. Machumu alisema uwapo wa utekelezaji familia ndani ya Wilaya ya Nanyumbu, ni tatizo ambalo limekuwa likishika kasi hasa katika kipindi cha msimu wa korosho.

Alisema kutokana na hali hiyo katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita, familia 40 hadi 50 zilitelekezwa na kusababisha baadhi ya athari.

Machumu alizitaja baadhi ya athari zilizojitokeza baada ya familia hizo kutelekezwa ni chuki, maradhi na watoto kukosa haki zao za msingi.

Alisema jamii inatakiwa kutambua kuwa vinapotokea vitendo hivyo vya ukatili wa kijinsia waathirikia wakubwa ni wanawake na watoto, hivyo kuna kila sababu ya kupinga vitendo vya aina hiyo.

"Ndoa nyingi zinakuwa na ushirikiano mzuri katika kipindi maisha yanakuwa magumu, lakini unapokuja msimu wa korosho na mazao mengine wakati wa mavuno, na hasa mmoja anapolipwa fedha basi ndoa inaingia mgogoro na kuvunjika," alisema Machumu.

Jafari Milanzi, mzazi wilayani Nanyumbu, alisema wapo baadhi ya wanaume ambao kipindi cha malipo ya korosho wamekuwa wakitelekeza famil-




Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri (katikati), akisikiliza maelezo kutoka kwa Meneja Misitu wa Kampuni ya Tumbaku ya JTI Leaf, Alfadhil Makengo, wakati wa uzinduzi wa upandaji miti kwa vyama vya msingi vya wakulima Mkoa wa Tabora. Wengine kutoka kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Abel Busalama na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, Dk. John Pima. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# JTI Leaf yazindua mradi mkubwa wa upandaji miti

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Tumbaku ya JTI Leaf, imezindua kampeni maalumu ya upandaji miti yenye lengo la kupanda miti zaidi ya milioni tano katika mkoa wa Tabora na Shinyanga ifikapo Desemba 16 na 17.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, alipongeza JTI Leaf kwa jitihada hizo na kusema mradi huu hautapendezesha tu Mkoa wa Tabora bali utasaidia katika utunzaji wa mazingira.

"Mradi huu ni endelevu na utakuwa unafanyika kila mwaka sisi kama serikali tutakuwapo kusimamia kikamilifu kwa juhudi kama hizi zinaunga mkono juhudi za serikali za kuhakikisha wananchi wanapanda miti na kuitunza," alisema na kuongeza kuwa kumekuwa na uharibifu mkubwa mno wa mazingira kwa kukata miti ovyo.

Alitoa wito kwa wakazi wa Tabora hususan wakulima kwa kupitia vyama vyao vya msingi kuhakikisha mradi huu unafanikiwa na pia wakumbuke kuitunza miti watakayoipanda.

"Hapo awali tulikuwa tunaotesha tu miti na kuiacha ikue yenyewe bila kuitunza ila kwa kupitia mradi huu wa JTI miti mingi itapona huku akiwataka viongozi wa mkoa huo kuhakikisha mradi huu unatekelezwa vikamilifu na takwimu sahihi ya miti iliyopandwa inachukuliwa vizuri."

Naye Meneja Misitu wa JTI Leaf, Alfadhil Makengo, ambaye aliongozana na Meneja Mahusiano na Mawasiliano wa JTI Leaf, Bright Kiwia, alisema mradi huo utatekelezwa katika vyama vya msingi 43 mkoani Tabora na Shinyanga.

Alisema pamoja na uzinduzi huo, lakini zoezi la upandaji limeshaanza katika maeneo mengi na kwamba Desemba 16 na 17 itakuwa kilele na kwamba zoezi hili litafanyika kila mwaka.

"Kuanzia msimu wa 2017/18 hadi sasa tumeotesha zaidi ya miti milioni 7 na lengo ni kufanya mradi huu uwe endelevu," alisema.

Kwa upande wake, Bright Kiwia, alisema pamoja na kununua tumbaku, kampuni ya JTI Leaf itaendelea kuhamasisha wakulima kuhusu upandaji miti na utunzaji wa mazingira kwa ujumla.

Mkuu wa Wilaya ya Kaliua, Abel Busalama, alisema ofisi yake itahakikisha mradi huo unatekelezwa kwa ukamilifu na kuipongeza JTI Leaf kwa kuunga mkono juhudi za serikali za upandaji miti ikiwa ni mojawapo ya namna ya kutunza mazingira.

# Zanzibar kupanua mkongo wa taifa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar ipo mbioni kupanua miundombinu ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kuhakikisha kuwa maeneo yote ya pembezoni na vijiji vyote hapa visiwani vinanufaika na huduma hii.

Hatua hiyo ni sehemu ya mkakati mpana na kabambe wa kufanikisha teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama) inatoa mchango stahiki katika ukuaji wa uchumi na pia Tehama inakuwa ni kitovu cha huduma visiwani.

Akizungumza na waandishi wa habari kutoka Tanzania Bara wapo visiwani humo kujifunza namna Tehama ilivyo chagiza maendeleo ya uchumi na kijamii, Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano Zanzibar, Mhandisi Shukuru Awadhi Suleiman, alisema upanuzi wa miundombino utatoa fursa kwa Wazanzibari wote kwa ujumla wake.

"Mpango wa upanuzi wa miundombinu utapita katika barabara zote mpya zilizojengwa hivi karibuni maeneo ya Unguja na Pemba," alisema.

Suleiman alisema na kupongeza mchango wa wabia na wadau mbalimbali katika sekta ya Tehama.

Alisema Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano unapata teknolojia na utaalamu kutoka kampuni kubwa ya kichina ya mawasiliano ya ZTE Corporation inayotoa mchango mkubwa katika ukuaji wa sekta hiyo.

"Huu ni mradi unaoendelea na popote barabara mpya inapojengwa na sisi tunakwenda huko," alisema Mhandisi Suleiman.

Alisema juhudi zinafanywa kuhakikisha kuwa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano utazifikia au kuunganishwa na taasisi zote za serikali katika ngazi zote na kwamba mpango huu ulianza kutekelezwa Agosti 6, 2019.

"Kwa sasa tupo Mfenesini-Mkokotoni katika Barabara ya Unguja Kaskazini ambako zinaendelea kujengwa," alisema bila kutaja gharama halisi ya mradi huo.

Alisema mpaka sasa taasisi za serikali zaidi ya 120 zimeshaunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na hivyo kunufaika na huduma za Tehama kwa kuongeza ufanisi wa kazi.

"Hizi taasisi za serikali zaidi ya 120 zinajumuisha ofisi 11 za wilaya za Wakala wa Usajili wa Vitambulisho vya Ukazi, Ndoa, Talaka, Uzazi na Vifo," alisema Mhandisi Suleiman.

Aliongeza pia kuwa taasisi hizo pia zimeunganishwa kwenya kituo cha data cha eneo la Mazizini, Unguja kama sehemu ya mwendelezo mpango wa biashara.

## Shambulio Niger laua wanajeshi 73

**NIAMEY, Niger**

WANAMGAMBO wamewaua takriban wanajeshi 73 katika shambulio dhidi ya kambi moja ya kijeshi magharibi mwa Niger, kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na jeshi.

Wanajeshi 12 pia walijeruhiwa katika shambulio hilo likiwa baya zaidi kwa miaka kadhaa lililotokea Jumanne wiki hii.

Waziri wa Niger, Issoufou Katambe, aliaimbia BBC kwamba idadi kubwa ya magaidi 'imezuiliwa', hakuna kundi lililosema lilihusika na mauaji hayo, lakini wapiganaji wanaohusishwa na Islamic State na wale wa Boko Haram wanatekeleza operesheni zao nchini humo wanahusishwa na mauaji hayo.

Katambe aliongeza kuwa kulikuwa na mapambano makali katika eneo la Inates karibu na mpaka na Mali na kwamba mamia ya wapiganaji walishambulia kambi hiyo.

Shambulizi hilo lilifanyika umbali wa maili 30 kutoka Ouallam, ambapo wanajeshi wanne wa Marekani walifariki pamoja na wanajeshi wengine wanne wa Nigeria miaka miwili iliyopita wakati doria yao iliposhambuliwa katika uvamizi.

Wapiganaji wa Kiislamu wamekuwa wakifanya mashambulizi katika eneo lote la Jangwa la Sahara, wakiwateka raia wa kigeni na kulenga michezo inayopendwa sana na wageni hao.

Jeshi lililobuniwa kuweka usalama katika eneo hilo limeshindwa kuzuia ghasia hizo. Baadhi ya wachambuzi walisema kwamba uvamizi wa kambi za kijeshi unalenga sio tu kuiba silaha, lakini kupanua ardhi inayomilikiwa na Wanajihad hao.

Shambulio hilo lilijiri siku kadhaa kabla ya kufanyika kwa mkutano nchini Ufaransa kati ya Rais Emmanule Macron na viongozi wa mataifa ya Afrika Magharibi kuzungumzia usalama katika eneo hilo.

Serikali ya Niger mapema iliomba kuongezewa muda wa miezi mitatu ili kutangaza hali ya tahadhari, ambayo mara ya kwanza ilitangazwa miaka miwili iliopita.

Jeshi la Niger linang'ang'ania kudhibiti kuenea kwa makundi yalioji-hami hata hivyo katika wiki za hivi karibuni kumekuwa na mashambulio yaliyoongezeka kutoka kwa washirika wa kundi la Islamic State katika eneo la taifa hilo lililo karibu na Mali.

Wapiganaji wanaoendesha operesheni zao katika eneo hilo na Niger ni wanachama wa kundi la mataifa matano ya Sahel G5 - pamoja na Burkina Faso, Mali, Mauritania na Chad ambayo inalenga kukabiliana na mashambulizi hayo.

Kwa mujibu wa Reuters wanajeshi watatu na wapiganaji 14 waliuawa Jumatatu katika shambulio dhidi ya kambi nyingine katika eneo la Agando magharibi mwa Jimbo la Tahoua, Wizara ya Ulinzi ilisema.

Maelfu ya raia na wanajeshi wameuawa katika eneo hilo la Sahel ambako mapigano hayo yalianza wakati wapiganaji walipoasi Kaskazini mwa Mali mwaka 2012.

Mgogoro kwa sasa umeenea hadi katikati mwa Mali na nchi jirani za Burkina Faso na Niger.

BBC




Waziri Mkuu Boris Johnson alifika kituoni huku akisindikizwa na mbwa wake. **PICHA: DW**

# Uchaguzi Uingereza watu wajitokeza kote

**LONDON,** Uingereza

RAIA wa Uingereza wanapiga kura katika uchaguzi mkuu wa tatu unaofanyika katika muda usiotimia miaka mitano.

Uchunguzi wa maoni unaonyesha kuwa chama cha Conservative cha Waziri Mkuu Boris kinao uwezekano wa kushinda.

Licha ya baridi kali na mvua za rasharasha, mistari mirefu ya wapigakura inaonekana katika vituo vya kupigia kura nchini kote Uingereza. Vituo katika majimbo yote 650 ya England, Scotland, Wales na Ireland ya Kaskazini vimefunguliwa saa moja asubuhi, na vinatarajiwa kufungwa rasmi saa nne usiku, majira ya Uingereza. Waziri Mkuu Boris Johnson amepiga kura mjini London, akisindikizwa na mbwa wake.

Viongozi wa kisiasa wametumia mtandao wa twitter kuwahimiza watu kwenda vituoni na kuvichagua vyama. Boris Johnson wa Conservative amesema hii ni fursa ya kuhakikisha kwamba mchakato wa Brexit unakamilika, na katika ujumbe wake wa kuhitimisha kampeni hapo jana, aliwataka Waingereza kuweka kando tofauti zao na kumwezesha kulitimiza hilo.

Bila kujali mtazamo wako, bila kujali kama uliunga mkono kubaki au kuondoka katika Umoja wa Ulaya, huu ni wakati wa kuja pamoja na kusonga mbele na kuheshimu matakwa ya watu wa nchi hii." Alihimiza Johnson.

Kwa upande wake kiongozi wa chama kikuu cha upinzani cha Labour, Jeremy Corbyn, alisema kura kwa chama chake ni kura ya kumaliza sera ya kubana matumizi. Katika ujumbe wake wa kukamilisha kampeni, Corbyn alisema katika maeneo yote aliyokwenda, alitetea maslahi ya watu wa kawaida.

Alisema, "Ujumbe ulikuwa ule ule, tunataka haki, tunataka haki na fursa sawa. Hatutaki nchi inayoendeshwa na matajiri na mabilioni na kuwasahau wengine."

Uchunguzi wa maoni ya wapigakura unampa nafasi kubwa Johnson na chama chake cha Conservative kupata ushindi, lakini matokeo rasmi ndiyo yatakayoonyesha ikiwa ataweza kupata viti vya kutosha kupitisha maamuzi yake bungeni.

Ikiwa Johnson atashindwa kupata wingi huo, wachambuzi wa siasa za Uingereza wanazungumzia uwezekano wa vyama vidogo kupata kura ya turufu, juu ya kuamua namna ya utawala utakaoundwa kutokana na ushirikiano wa kivyama.

Vyama hivyo ni pamoja na chama cha kiliberali, Liberal Democrats kinachoongozwa na Bi Jo Swinson, ambacho kimeshikilia msimamo imara wa kutaka kuibakisha Uingereza ndani ya Umoja wa Ulaya, na hivyo kinaweza kuvutia wapiga kura wasiopenda mchakato wa Brexit.

Katika uchaguzi uliopita mwaka 2017, chama cha Conservative kililazimika kushirikiana na chama cha DUP cha Ireland ya Kaskazini, kuweza kupata viti vya kutosha kuunda serikali.

Kura zitaanza kuhesabiwa saa 4:00 usiku mara baada ya vituo kufungwa. Matokeo mengi yanatarajiwa kutangazwa mapema Ijumaa asubuhi.

Jumla ya wabunge 650 watachaguliwa kwa kutumia mfumo wa 'first-past-the-post' unaotumika kwenye uchaguzi mkuu, ambao wapiga kura huchagua yule wanayemtaka, na mgombea atakayepata kura nyingi zaidi ndiye atakayeibuka mshindi.

**BBC**

# Maelfu ya watu wapuuza amri ya kutotoka nje India

**DELH, India**

MAELFU ya watu wameshiriki katika maandamano ya kupinga sheria ambao inawapa uraia watu wasio Waislamu kutoka nchi jirani na hivyo kuipuuza amri ya kutotoka nje kwenye Jimbo la Assam, Kaskazini Mashariki mwa India.

Muswada wa marekebisho ya uraia, ambao unaahidi kuwapa uraia jamii ya watu wachache ya Wahindu, Buddha, Jain, Waparsi na Wakristo ambao wanakimbia mateso ya kidini katika nchi zenye Waislamu wengi kama vile Pakistan, Bangladesh na Afghanistan, ulipitishwa juzi na Bunge.

Waandamanaji walikusanyika kwenye maeneo mbalimbali ya Guwahati mji mkubwa katika Jimbo la Assam na kuchoma matairi, kurusha mawe na kuimba nyimbo kabla ya kutawanywa na polisi.

Wakosoaji wa muswada huo walisema ni kinyume cha maadili yaliyowekwa na katiba ya India isiyo na dini kwa kuifanya dini kama msingi wa uraia. Pia walisema inawabagua Waislamu.

**DW**

# Hatimaye Malinzi aachiwa huru

**Na Hellen Mwango**

HATIMAYE Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Jamali Malinzi (60) na aliyekuwa Katibu Mkuu wake, Selestine Mwesigwa (49), waliachiwa huru jana katika Gereza la Keko, baada ya kukamilisha kulipa faini jumla ya Sh. milioni 1.5.

Juzi, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, iliwahukumu kulipa faini ya jumla ya Sh. milioni 1.5 au kwenda jela kutumikia kifungo cha jumla miaka minne kwa makosa mawili ikiwamo kosa la kughushi muhtasari wa kubadilisha watia saini wa akaunti za TFF kwamba Kamati Tendaji imepitisha mabadiliko hayo.

Kosa la pili, imemtia hatiani Mwesigwa kwa kosa la nne la kuwasilisha muhtasari wa kughushi benki kwa ajili ya kubadilisha watia saini.

Hakimu Mkazi Maira Kasonde, aliyesikiliza kesi hiyo, alisema kosa la kughushi muhtasari washtakiwa wote wawili watalipa faini ya Sh. 500,000 au kwenda jela miaka miwili wote wawili, na kosa la nne mshtakiwa Mwesigwa atalipa faini ya Sh. 500,000 au kwenda jela miaka miwili.

Hata hivyo, vigogo hao wametumikia kifungo hicho siku moja, na walifanikiwa kulipa faini hiyo jana asubuhi.

Awali, akiichambua hukumu hiyo, hakimu alisema upande wa Jamhuri umeshindwa kuthibitisha makosa 18 kati ya 20, ikiwamo ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha fedha.

"Mahakama yangu imewatia hatiani kwa makosa mawili kosa la tatu linawakabili wote wawili kila mshtakiwa atalipa faini ya Sh. 500,000 au jela miaka miwili na la nne linamkabili Msigwa peke yake, atalipa faini ya Sh. 500,000 au kwenda jela miaka miwili," alisema na kuongeza:

"Katika mashtaka ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha fedha, mahakama yangu imeona hakuna ushahidi wa Jamhuri uliothibitisha makosa hayo dhidi ya washtakiwa," alisema.

Akiichambua hukumu hiyo hakimu alisema kuhusu hoja za mshtakiwa kuikopesha fedha TFF ni kweli alitoa fedha hizo, lakini anaungana na Jamhuri kwamba hakufuata taratibu za shirikisho hilo kuhusu mkopo kutoka kwa mtu binafsi.

Juni 29, 2017 Malinzi na wenzake wawili walifikishwa katika mahakama hiyo wakikabiliwa na mashtaka 28 ikiwamo ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha fedha.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, akipokelewa na Ofisa Biashara Mkuu wa Benki ya CRDB, Dk. Joseph Witts alipowasili katika kongamano la uwezeshaji kwa makandarasi na wazabuni kwa mikoa ya Shinyanga, Geita, Kigoma na Tabora lililoandaliwa na Benki ya CRDB, kongamano hilo limefanyika ukumbi wa mikutano wa NSSF, mjini Shinyanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC apiga marufuku viboko, ataka wapande miti

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

SERIKALI mkoani Katavi imeagiza kufutwa adhabu ya viboko kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika Kata ya Mwese Wilaya ya Tanganyika, badala yake wapewe adhabu ya kupanda miti.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, alitoa agizo hilo jana katika kikao cha kamati ya ushauri ya mkoa (RCC), kilichofanyika mjini Mpanda.

Homera alisema kuwa kuna zaidi ya miti milioni moja ambayo imeoteshwa kwenye Kata ya Mwese na inatolewa bure hivyo kila mwanafunzi anayetakiwa kupewa adhabu ya kuchapwa viboko asichapwe, badala yake awe anapewa adhabu ya kupanda miti.

Alisema kuwa agizo la kupanda miti pia amelitoa kwa wakazi wa kata hiyo na mwananchi ambaye atapatikana hajapanda miti atachukuliwa hatua za kisheria.

Alisema kuwa ameshatoa agizo kwa Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika kuhakikisha askari wa jeshi la akiba wanafanya msako na kuwabaini watu ambao watakuwa wamekaidi agizo hilo la kupanda miti ya misindano.

Alisema agizo hilo likitekelezwa kikamilifu litawafanya wakazi wa kata hiyo baada ya kipindi cha miaka sita kuanza kuvuna miti hiyo na kujipatia kipato kikubwa lengo la mkakati huo ni kutaka watu kujiongezea kipato na kuboresha maisha yao.

Pia aliwataka watumishi mbalimbali wa mkoa huo kuboresha utendaji kazi kwa kuwa wapo baadhi ya watumishi ambao hata wanapokuwa likizo hawapigiwi simu, hivyo wajue kuwa wao ni mizigo kwenye sehemu zao za kazi.

Alisema mtendaji mzuri wa kazi anapokuwa amekwenda likizo watumishi wenzake wanamkumbuka kwa utendaji wa kazi na lazima apigiwe simu ya kuulizwa atarudi lini.

Naye Meya wa Manispaa ya Mpanda, Willy Mbogo, aliwashauri watumishi ambao muda wao wa kustaafu unakaribia kutumia vizuri fursa hiyo ya kupanda miti hiyo inayotolewa bure.

Alisema mti mmoja wa msindano unauwezo wa kuvunwa na kutoa mbao zenye thamani ya Sh. 45,000, hivyo mtu akitunza vizuri miti yake kila mwisho wa mwezi anavuna miti na kujilipa mshahara kila mwezi.

Baadhi ya wajumbe wa kikao hicho walizungumzia changamoto ya kuwapo na tabia ya uchomaji moto ovyo kwenye mashamba ya miti hali inayoanza kuwavunja moyo kupanda miti kwenye mashamba yao.

Padri Anacretus Bafumkeko alishauri kuwa mkoa wa Katavi uandae mkakati na mpango wa kuhakikisha tatizo la upungufu wa matundu ya vyoo kwenye shule za sekondari na msingi linakwisha.

Alisema endapo utaanzishwa utaratibu wa wadau mbalimbali kuchangia kwenye elimu kutafanya wanafunzi wewe wanatumia vyoo bora na vya kisasa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mpimbwe, Nyasongo Serengeti, aliomba Kata ya Majimoto yenye wakazi wapatao 39,000 ambao wanatumia huduma ya zahanati ambayo imezidiwa wajengewe kituo cha afya.

# Serikali kuwezesha ukataji bima maisha

**Na Beatrice Moses**

JUHUDI za kuboresha na kuinua vipato vya wananchi zinazofanywa na Serikali, zinatajwa kuwa zikifanikiwa inaweza kuwa ni hatua nzuri ya kuhamasisha wananchi wengi kukata bima ya maisha.

Kamishna wa Mamlaka ya Bima Tanzania (Tira), Dk. Mussa Juma, aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa chama cha Wakala wa Bima nchini jijini Dar es Salaam.

Dk. Juma alisema wenye kipato kidogo kufikiri kukata bima ya maisha ambayo ni sawa na uwekezaji, wakati hawana uhakika wa kupata chakula na kulala.

"Duniani pote zipo bima za aina mbalimbali, kuna bima ambazo ni za lazima mwananchi analazimishwa kukata bima hata kama anataka au hataki na hiari ya mtu, bima ni kama bidhaa nyingine," alisema.

Alisema kwa sababu nchi inakwenda kwenye uchumi wa kati, hivyo anaamini kipato kitaongezeka wananchi wengi watakuwa na uwezo wa kukata bima za aina mbalimbali.

Aliwataka mawakala hao kuhakikisha wanakitumia vyema chama hicho ikiwamo kushiriki kikamilifu katika kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kukata bima.

Alisema pia bima ni ulinzi wa mali zikiwamo za viwandani, hivyo katika kutimiza azma ya Serikali, wamiliki wa viwanda wanapaswa kuona umuhimu wa kukata bima hizo.

"Mawakala jukumu lao kubwa ni kuunganisha wateja na makampuni ya bima, hivyo wana umuhimu katika kukuza na kuza huduma hiyo ambayo kwa upande mwingine ni bidhaa," alisema Dk. Juma.

Mwenyekiti wa chama hicho, Sayi Daudi, alisema wanafurahi kufanikiwa kuanzisha chama hicho ambacho kitawasaidia kufanya kazi yao kwa ushirikiano wenye manufaa ya jumla kwenye sekta hiyo.

Daudi alisema kwa kawaida mawakala wamekuwa na jukumu la kuunganisha wateja na kampuni hadi kufikia hatua ya kuandikiana mikataba.

Meneja masoko wa Kampuni ya Bima ya Icea Lion, Davis Mwijage, alisema miongoni mwa mambo yatakayosaidia mafanikio ya utekelezaji wa sera ya uchumi wa viwanda ni pale mwekezaji atapokata bima ya ulinzi wa mali zake hivyo kuwa na amani.

"Hatua hiyo itampa amani moyoni mwake kwamba hata akipatwa majanga atafidiwa na bima," alisema.

Miongoni mwa juhudi zinazofanywa na serikali kuimarisha uchumi ni kujenga miundombinu zikiwamo barabara na reli ya kisasa.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**KAZI /AJIRA**

**Nafasi za kazi** ualimu masomo ya sst/diploma 0656490706/0784142792

***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**au piga simu: 0782253676**


IN THE DISTRICT DELEGATE MAGISTRATE COURT OF MBINGA
AT MBINGA
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO 10 201 9
IN THE MATTER OF ESTATE OF THE LATE GIDO MOSES NKOLELA
AND
IN THE MATTER OF APPLICATION FOR APPOINTMENT OF ADMINISTRATION OF THE ESTATE OF THE LATE GIDO MOSES NKOLELA
BY
MARIA PHILIMIN NDUNGURU

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they thing fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 06 day of 01 2020

The will to the said is deposited and open for inspection at the Court.
Dated at MBINGA this 20 Day of 11 2019

The Magistrate in Charge
DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE
MBINGA

215554702

**Primary Court (Administration of Estates)**

**FORM II**

**Citation**

**Katika Mahakama ya Mwanzo MABIRA**

**Usimamizi wa Mirathi No. 15/2019**

**Ombi la JOVENARIUS KIIZA JOHN kuteuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi ya Marehemu JOHN BATISITA KAYANDA.**

**KWA WATU WOTE KARAGWE NA KYERWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo mnaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 13/01/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe: 04/12/2019.

SAHIHI YA HAKIMU

15554502

**KUPOTEA KWA CHETI**



**Elias Lucas Kiondo** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0584/0042** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2003 katika shule ya Sekondari Lwandai. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAW/RB/437/2018**

215554302


***Uza, Chenye Thamani***

***Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Robertson: Kila timu inaihofia Liver Uefa




**NYON,** Uswisi

ANDY Robertson amesisitiza Liverpool imerudisha heshima yake Ulaya ambayo inaifanya timu nyingi kuiepuka kwenye hatua ya mtoano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Wekundu hao ndio mabingwa mtetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na waliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Salzburg 2-0 na kufuzu hatua ya mtoano wa timu 16 kwenye michuano hiyo mjini Nyon.

Kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp kiliifunga Tottenham 2-0 kwenye fainali ya michuano hiyo msimu uliopita, mwaka mmoja baada ya kupoteza kutoka kwa Real Madrid.

Ikiwa imemaliza kinara wa Kundi E, Liverpool inaweza kukutana na moja kati ya Real Madrid, Atalanta, Atletico Madrid, Borussia Dortmund au Lyon kwenye hatua ya mtoano.

Robertson anaamini kwamba timu zote zinataka kuiepuka Liverpool kwenye hatua hiyo kwa sababu ni bingwa mtetezi.

"Hiyo ndio hali halisi, miaka miwili iliyopita tulionyesha nafasi nzuri ambayo imeifanya kila timu kutuhofia," alisema Robertson akiwaambia waandishi wa habari.

"Pengine msimu wa kwanza wakati tulipokwenda kwenye fainali, sidhani kama tulikuwa tunaheshima vizuri, lakini baada ya kwenda Porto ndio tukapewa heshima."

# Lampard ajipanga kumnasa Sancho



**LONDON,** England

FRANK Lampard amesisitiza kwamba Chelsea itafanya kila inaloliweza kumnasa Jadon Sancho kwenye dirisha la Januari, kwa mujibu wa ESPN.

Ada ya mchezaji huyo wa Borussia Dortmund, Sancho mwenye umri wa miaka 19 ni pauni milioni 100.

Chelsea bado haijapata mtu wa kuziba pengo la Eden Hazard tangu alipoondoka kwenye dirisha lililopita kitu kinachomfanya kocha Lampard kuamini Sancho anaweza kwenda kumaliza tatizo hilo lililoachwa na supastaa huyo wa Kibelgiji aliyetimkia Real Madrid.

Lampard alisema: "Nadhani itakuwa safi sana na kumekuwa na majadiliano kuhusu tunavyoongeza nguvu kwenye kikosi chetu. Tulipoteza mabao mengi na asisti nyingi kwa kuondoka Eden. Tunahitaji mtu wa kumwongeza kwenye kikosi chetu kwa ajili ya eneo hilo."

Winga Wilfried Zaha naye amekuwa kwenye mipango ya klabu hiyo ya Stamford Bridge, ambayo juzi waliichapa Lille ya Ufaransa na kufuzu hatua ya mtoano ya 16-bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Sancho kwenye soka la England aliwahi kuichezea Manchester City.




# Neymar katika rada za Liver

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Liverpool wametajwa kuwa miongoni mwa klabu sita zinazotaka kumsajili Neymar.

Kwa mujibu wa Le Parisien, klabu vigogo wa huko Ulaya wakiwamo Liverpool wanamtazama Neymar kama chaguo lao la kwanza sambamba na staa mwenzake wa huko Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe.

Kwenye Ligi Kuu England, Liverpool wataungana na wapinzani wao Chelsea na Manchester City wanaohitaji saini ya mchezaji huyo, huku huko Hispania saini ya mchezaji huyo inawindwa na vigogo Real Madrid na Barcelona na Italia kuna Juventus ndio walioonyesha dhamira ya kumtaka.

Vita hiyo ya kunasa saini ya Neymar ni kama ya kinchi, ambapo England, Hispania na Italia zinachuana kunasa saini yake.

Hata hivyo, wachambuzi wa mambo ya soka wanadai kwamba Neymar atakapoamua kuachana na PSG basi mpango wake ni kurudi zake Hispania, mahali ambako alitamba na kikosi cha Barcelona kabla ya kuvunja rekodi ya dunia ya pauni milioni 198 aliponaswa na miamba hiyo ya Paris.

Huko Nou Camp kumekuwa na maelezo kwamba supastaa namba moja wa Barcelona, Lionel Messi anahitaji Mbrazil huyo akakipige kwenye kikosi chao huku kwa wapinzani wao, Barcelona, beki wa kushoto, Marcelo anamtaka Mbrazil mwenzake wakaungane pamoja kukipiga katika kikosi hicho cha 'Los Blancos'.



# Mourinho aitamani tena Bayern Uefa

**LONDON,** England

JOSE Mourinho ana matumaini kwamba, Tottenham inaweza kupata nafasi nyingine kuikabili Bayern Munich kwenye "mchezo mkali" wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, walipata ushindi wa 3-1 dhidi ya Spurs mjini Munich Jumatano na kuwa na kiwango kizuri kwenye Kundi B.

Ushindi huo umekuja miezi miwili tu baada ya Bayern kuifumua Tottenham mabao 7-2 jijini London, lakini kocha mkuu wa Spurs, Mourinho angependa tena kukutana na miamba hao wa Ujerumani.

"Matarajio yangu (kuja tena) kama tukija itakuwa ni robo fainali au nusu fainali kwa sababu hatuwezi kucheza na Bayern kwenye raundi inayofuata," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Matarajio yangu ni kurudi tena hapa kwenye mechi kali, ambayo ningependa itokee tena."

Mourinho, ambaye alichukua mikoba ya kuinoa Spurs mwezi uliopita, alisema alijaribu kuepuka kichapo walichokipata cha mabao 7-2.

"Nilijaribu kupuuzia kile kilichotokea kwenye mchezo wa kwanza. Nilijaribu kufikisha kutoka kwa wachezaji," alisema.

"Sikutaka kuonyesha taswira ya hilo. Sikuwaelezea wachezaji chochote kuhusu mchezo ule, lakini ilikuwa muhimu kwa upande wetu kuja hapa na kupata matokeo."




## Ronaldo, Higuain wamkuna Buffon

**TURIN,** Italia

GIANLUIGI Buffon amewasifia Cristiano Ronaldo na Gonzalo Higuain kwa kuonyesha mfano wakati Juventus ikiibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya Bayer Leverkusen kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumatano.

Juve tayari walikuwa wanaongoza Kundi D wakati wakielekea kwenye mchezo huo dhidi ya Leverkusen, ambao walihitaji kuepuka kipigo ili kuwa na nafasi ya kufuzu hatua ya 16-bora.

Vijana hao wa Peter Bosz walikuwa na kiwango bora kwenye kipindi cha kwanza, lakini Ronaldo alifunga kwa pasi ya Paulo Dybala dakika ya 75 na Higuain akafunga la pili na kuwatupa Wajerumani hao kwenye Ligi ya Europa.

Buffon alimsifia Ronaldo na Higuain kwa kuwaonyesha wachezaji wenzao wanatakiwa kujituma kwenye kila mchezo kwa msimu wote.

"Kama tunacheza mechi kwa staili hii, nina uhakika tunaweza kufanya vitu vikubwa. Hata hivyo, kama tunaingia kwenye mchezo kwa kusuasua, hilo litakuwa ni tatizo," Buffon alisema akiiambia Sky Sport Italia.

"Ni ishara mbaya kama huendi kwenye mechi bila kujitathmini na nina imani mambo yatakuwa sawa.

"Ninafurahi kwamba tulipata mfano kutoka kwa Higuain na Ronaldo kwenye kiwango na walijitolea kwa kuitumikia timu vizuri."

# Tuchel akunwa Neymar kumpa Cavani penalti




**PARIS,** Ufaransa

BAADA ya Neymar kumpa Edinson Cavani nafasi ya kupiga penalti dakika za mwisho, imethibitisha Paris Saint-Germain wanacheza kitimu zaidi, kwa mujibu wa kocha Thomas Tuchel.

PSG walikuwa na wakati mzuri kwenye mchezo wa Kundi A wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kuichakaza mabao 5-0 Galatasaray kwenye Uwanja wa Parc des Princes Jumatano.

Nyota wa kimataifa wa Brazil, Neymar alicheza vizuri na kutengeneza mabao mawili na yeye kufunga moja.

Neymar angeweza kufunga bao lake la pili kwenye mchezo huo, baada ya Kylian Mbappe – ambaye aliifunga bao la nne kwa PSG, alidondoshwa chini na Ryan Donk eneo la hatari.

Mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona alichukua mpira na kumpatia Cavani, ambaye hakufanya makosa na mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay, alimpeleka kushoto golikipa, Fernando Muslera na mpira kwenda kulia na kufunga bao lake la kwanza tangu Agosti.

Cavani na Neymar waliwahi kukwaruzana kwenye mchezo dhidi ya Lyon wakigombea kupiga penalti jijini Paris mwaka 2017.

Lakini sasa wachezaji hao wameonekana kupevuka na sasa kuachiana kupiga penalti kwa zamu.

"Ilikuwa ni ishara nzuri," alisema Tuchel akiwaambia waandishi wa habari.

"Kila mmoja anaweza kuona, Ney yupo makini. Alimpa mpira Edi na ishara nzuri kwa timu nzima.

"Neymar tayari alikuwa mchezaji muhimu kwa timu wakati tukishinda 3-1 dhidi ya Montpellier Jumamosi."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI ATESEKA NA MZIMU WA LIVER MTOANO UEFA

● ● ● Lazima tusahau nini kilichotokea mwaka jana na mwaka mmoja kabla, itakuwa ni makosa kufikiri...

**Barcelona,** Hispania

Lionel Messi amekiri kwamba Barcelona bado wanaendelea kuteseka na mzimu wa kutolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika misimu miwili iliyopita, lakini lazima "waanze kuanza" msimu huu

Barca ilitolewa kwa faida ya mabao ya ugenini Aprili 2018 baada ya kuongoza kwa tofauti ya mabao 4-1 dhidi ya Roma kwenye hatua ya robo fainali, lakini ikajikuta ikikubali kipigo cha mabao 3-0 katika mechi ya marudiano kwenye Uwanja wa Stadio Olimpico.

Kisha Liverpool ilipindua matokeo ya mabao matatu waliyofungwa na 'Blaugrana' hao katika hatua ya nusu fainali msimu uliopita kwa kuichapa 4-0 katika Uwanja wa Anfield, na Messi anakiri maumivu ya vipigo hivyo bado ni makali kwao.

**Barca imemaliza kileleni mwa Kundi F ambalo msimu huu lilikuwa kizijumuisha Borussia Dortmund, Inter na Slavia Prague, na Messi amewataka wenzake kusahau kuhusu kilichotokea katika michuano iliyopita wakati hatua ya mtoano itakapoanza Februari mwakani.**

"Kwa kuwa mkweli, mara zote maumivu yapo," mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or alisema kuhusu machungu ya kutolewa Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati wa sherehe za Adidas juzi, Jumatano.

"Lakini tunapaswa kuanza tulipoumizwa. Ni mwaka mpya, mashindano mapya. Ni wazi tunapaswa kujifunza kutokana na makosa, lakini kufikiri ya sasa na baadaye.

"Lazima tusahau nini kilichotokea mwaka jana na mwaka mmoja kabla, itakuwa ni makosa kufikiria hayo."

Droo ya hatua ya mtoano inatarajiwa kupangwa Jumatatu ijayo na licha ya mabingwa watetezi, Liverpool waliyoitoa Barcelona msimu uliopita, timu zote za Ligi Kuu England zimefuzu hatua hiyo ya 16-bora baada ya juzi Manchester City na Tottenham kuungana na Chelsea pamoja na miamba hiyo ya Anfield.

Timu zilizofuzu hatua 16- bora katika kila kundi ni; Kundi A: Paris St-Germain (vinara), Real Madrid (ya pili), Kundi B: Bayern Munich (vinara), Tottenham (ya pili), Kundi C: Manchester City (vinara), Atalanta (ya pili), Kundi D: Juventus (vinara), Atletico Madrid (ya pili).

Kundi E: Liverpool (vinara), Napoli (ya pili), Kundi F: Barcelona (vinara), Borussia Dortmund (ya pili), Kundi G: RB Leipzig (vinara), Lyon (ya pili) wakati Kundi H: Valencia wakiwa vinara na Chelsea ikimaliza nafasi ya pili.

## KWA UFUPI

### EVERTON YAMVAA IBRAHIMOVIC
Everton imezungumza na wakala Mino Raiola kuangalia kama mshambuliaji wa zamani wa Sweden, Zlatan Ibrahimovic, 38, atafungua milango ya kutua Goodison Park, ingawa AC Milan bado inapewa nafasi ya kumsajili straika huyo wa zamani wa Manchester United. (Arena Napoli, via Sport Witness)

### LAMPARD AMTAKA ZAHA JANUARI
KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard anajiandaa kwenda kumsajili winga wa Crystal Palace na Ivory Coast, Wilfried Zaha, 27, katika dirisha la Januari. (Mirror)

### ARTETA AFUNGUKA ARSENAL
KOCHA msaidizi wa Manchester City, Mikel Arteta, angependa kurudi klabu yake ya zamani ya Arsenal kuwa kocha, lakini anataka kuhakikishiwa kwanza kutoka kwa uongozi. (Sun)

### DORTMUND YAMFUATILIA POCHETTINO
Borussia Dortmund inafuatilia kwa karibu namna ya kumnasa kocha wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino, na kocha wao wa sasa, Lucien Favre yupo kwenye presha kubwa katika klabu hiyo ya Ujerumani. (Telegraph)

### BILIONEA MMAREKANI AITAKA CHELSEA
BILIONEA wa Marekani, Todd Boehly, ambaye pia anaimiliki Los Angeles Dodgers, anataka kutoa ofa mpya ya kuinunua Chelsea, licha ya klabu hiyo kusisitiza haiuzwi. (Telegraph)

### ANCELOTTI LULU EVERTON, ARSENAL
Arsenal na Everton zinajiandaa kukutana na kocha wa zamani wa Chelsea, Carlo Ancelotti, baada ya kutimuliwa na Napoli Jumanne usiku. (Evening Standard)

### UNITED KUMKOSA MADDISON
Leicester City inakaribia kumpa mkataba mpya wa muda mrefu kiungo wa England, James Maddison, 23, ambaye amekuwa akihusishwa na kujiunga na Manchester United. (Mirror)

### HAVERTZ AVUTIA VIGOGO ULAYA
Manchester United imeonyesha kuvutiwa na huduma ya kiungo wa Bayer Leverkusen, Mjerumani Kai Havertz, 20. Hata hivyo, itakabiliana na ushindani kutoka kwa Barcelona, Liverpool, Real Madrid na Bayern Munich. (Bild, via Express)

### AKE ATAKIWA CHELSEA JANUARI
FRANK Lampard pia anataka kumrejesha Chelsea beki wa kati wa Bournemouth, Nathan Ake, na tayari 'Blues' hao wameandaa pauni milioni 40 za kuununua mkataba wa Mholanzi huyo iliyomuuza kwa 'Cherries' hao mwaka 2017. (Guardian)

### ATLETICO, INTER KWA GIROUD
Inter Milan na Atletico Madrid ni miongoni mwa klabu zinazomuwinda Olivier Giroud, 33, ambaye yupo tayari kuondoka Chelsea ifikapo Januari. (Football. London)

### PELLEGRINI KUTIMULIWA JUMAMOSI
West Ham itamtimua kocha wao mkuu, Manuel Pellegrini, 66, kama klabu hiyo itapoteza mechi yake ya Jumamosi dhidi ya Southampton. (Sun)

### FERGUSON AKATAA JUMLA EVERTON
KOCHA wa muda wa Everton, Duncan Ferguson, 47, hataki kupewa kazi hiyo jumla licha ya kufanikiwa kuichapa Chelsea kwa mabao 3-1 katika mechi yake ya kwanza tangu alipokabidhiwa jukumu hilo la kuiongoza. (Liverpool Echo)

# AMRI SAID KUANZA NA YANGA MBEYA CITY

**Na Focus Nicus**

LICHA ya awali kuelezwa yupo mbioni kuingia mkataba na Ndanda FC, aliyekuwa Kocha wa Biashara United, Amri Saidi, amesaini mkataba wa miezi sita wa kuinoa Mbeya City ya jijini Mbeya.

Saidi anachukua mikoba ya Juma Mwambusi aliyejiuzulu hivi karibuni kuinoa timu hiyo na kuiacha ikiwa nafasi ya pili kutoka mkiani na pointi nane baada ya kushuka dimbani mara 12 msimu huu.

Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya ratiba ya Ligi Kuu yaliyotolewa juzi na Bodi ya Ligi, Said ataanza kuiongoza timu hiyo kwa kuialika Yanga kwenye Uwanja wa Sokoine Desemba 24, mwaka huu.

Akizungumza na mwandishi wetu kocha huyo aliyewahi pia kuinoa Lipuli FC na Mbao FC, alisema anatarajia kuanzia alipoishia Mwambusi na mkakati wake ni kukiboresha kikosi hicho kuelekea dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kufunguliwa Jumatatu ijayo.

"Kwanza kabisa kwa sasa sipendi kuzungumzia mechi dhidi ya Yanga, ingawa mchezo huo najua utakuwa mgumu kwani Yanga ni timu kubwa, mpango wangu ni kuanzia alipoishia Mwambusi na tayari nimeona tunahitaji kuimarisha kikosi kwa kusajili wachezaji wanne ama watano.

"Ninachokiomba kwa sasa ni wadau na Wanambeya wote kuniunga mkono na kuonyesha ushirikiano kwa kuisapoti timu hii ili iweze kufanya vizuri," alisema.

Kuelekea usajili wa dirisha dogo, ni wazi Saidi itabidi amulike zaidi safu yake ya ulinzi kwani inaonyesha ndio 'mdebwedo' zaidi kati ya timu zote 20 zinazoshiriki ligi hiyo kutokana na kuruhusu mabao (19) mengi zaidi kujaa katika nyavu zao hadi sasa msimu huu.

HEKAHEKA...




Mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo (kushoto), katika hekaheka za kutaka kufunga huku akipata upinzani kutoka kwa winga wa Bayer Leverkusen, Moussa Diaby, kwenye mechi ya mwisho ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyopigwa Uwanja wa BayArena, Ujerumani juzi na miamba hiyo ya Italia kushinda 2-0. **HABARI UK. 29.** **MPIGAPICHA WETU**

# Shime aipania Sudan U-17 Cecafa leo

**Na Somoe Ng'itu,** JINJA

NI zaidi ya fainali! Hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa timu ya wasichana wa umri chini ya miaka 17 ya Tanzania Bara, Bakari Shime, kuelekea mechi dhidi ya Sudan itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Njeru, Jinja nchini Uganda.

Mechi hiyo kati ya Tanzania Bara yenye pointi nne sawa na Kenya, inatarajiwa kuchezwa kuanzia saa 7:30 mchana na ili kurejea katika mbio za ubingwa wa mashindano hayo ya kwanza ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati itatakiwa kupata ushindi.

Akizungumza na Nipashe mjini hapa, Shime, alisema wamerekebisha makosa yaliyojitokeza katika mechi iliyopita na leo ndio fainali ya timu yake katika mbio za kuwania taji hilo la kwanza.

Shime alisema wanahitaji kupata ushindi na hilo linawezekana kwa kuwaandaa wachezaji wake kucheza katika kiwango chao cha kawaida huku akiwajenga kisaikolojia, wasahau mchezo uliopita.

"Kwetu kesho (leo), ndio tunaanza rasmi mashindano, ili tuweze kuibuka mabingwa, ni lazima tuwafunge Kenya, halafu Uganda, mechi ya mwisho itakuwa ni ya kukamilisha ratiba, nimekuwa na kikao kirefu na wachezaji na ninaamini, watarejea kucheza katika ubora wao tulioulizoea," alisema Shime.

Aliongeza kuwa wakicheza kwa utulivu, mechi hiyo itakuwa nyepesi na watapambana kuhakikisha wanatimiza malengo waliyojiwekea.

"Tutaingia katika mechi ya kesho kwa mtindo wa mtoano, tukiamini kuwa tukishinda tutakuwa bado tuna nafasi ya kutwaa ubingwa, lakini tukipata matokeo tofauti, nafasi yetu itakuwa finyu, sina majeruhi mpya na Emiliana [Mduma], anaendelea vizuri," Shime alisema.

Nahodha Irene Kisisa alisema wataingia uwanjani leo wakiwa makini zaidi na wamejipanga kupambana ili kupata matokeo mazuri.

"Tuliumia sana mechi dhidi ya Burundi, tumeona makosa yetu, tunaamini hatutarudia tena, tumejiandaa kupambana, lakini tunasema kuwa mashindano ni magumu, kila timu inapambana kusaka pointi," alisema nahodha huyo.

Mechi nyingine za mashindano hayo yanayochezwa kwa mtindo wa ligi, lakini mkondo mmoja itakuwa ni kati ya Djibouti dhidi ya Burundi huku Uganda yenye pointi sita na inaongoza katika msimamo ikiwakaribisha Eritrea yenye pointi moja.

## Samatta: Sababu kipigo Napoli hii

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa Kimataifa wa Tanzania na nahodha wa Taifa Stars, anayeichezea klabu ya KRC Genk ya Ubelgiji, Mbwana Samatta, amesema kipigo cha mabao 4-0 kutoka kwa Napoli FC ya Italia kwenye mechi ya mwisho ya kukamilisha hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, kilitokana na kutojiandaa kwa ajili ya michuano hiyo.

Katika Kundi lao E, Genk imemaliza mkiani ikiwa na pointi moja tu baada ya kupata sare moja na kupoteza mechi tano huku mabingwa watetezi, Liverpool wakimaliza kileleni na pointi 13 wakifuatiwa na Napoli wenye alama 12 na Salzburg iliyomaliza nafasi ya tatu ina pointi saba.

Akizungumzia mechi hiyo iliyopigwa katika Uwanja wa San Paolo nchini Italia, Samatta alisema si kweli kwamba walishuka dimbani ili tu kukamilisha ratiba kutokana na kupoteza nafasi ya kusonga mbele, bali walidhamiria kushinda ila kilichoonekana ni kutojiandaa vema kushiriki michuano hiyo mikubwa kwa ngazi ya klabu barani Ulaya.

"Kama ukiangalia utagundua tangu mwanzo timu ilikuwa haijajiandaa kwa michuano mikubwa kama hii ndiyo maana hatukuweza kufanya vizuri na si kweli kwamba tulishuka uwanjani kwa ajili tu ya kukamilisha ratiba," alisema mshambuliaji huyo ambaye amemaliza michuano hiyo akiwa na mabao matatu.

Katika mechi hiyo, Samatta alicheza kwa dakika 63 tu kabla ya kumpisha winga Theo Bongonda, ambaye hata hivyo kuingia kwake hakukuweza kusaidia kubadili matokeo.

## ZFF yafungua dirisha dogo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limefungua rasmi dirisha dogo la usajili ambalo limeanza tangu Jumanne Desemba 10, mwaka huu na litadumu hadi Januari 9, mwakani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati ya Mashindano ZFF, Hussen Ahmada alisema dirisha hilo la usajili litatoa fursa kwa klabu kusajili wachezaji kwa mujibu wa kanuni ya mashindano ya mwaka 2019/2020 kifungu 8(5).

Alisema dirisha hilo dogo halipaswi kuathiri mwenendo wa ligi za mikoa pamoja na zile za wilaya zinazoendelea kwa sasa.

Aidha, alizitaka klabu kulifanya zoezi hilo kwa wakati uliopangwa ili kuepusha usumbufu ikiwamo kuchelewa kurejesha fomu kwa muda uliopangwa.

"Klabu tunaomba wafuate taratibu na muda uliopangwa kwa ajili ya kufanya usajili wa kipindi hili cha dirisha dogo, zipo baadhi ya klabu kwa makusudi husubiri muda ambao ZFF utaongeza ndio zisajili na hii muda mwingine inatuletea usumbufu," alisema.

Michezo

Ijumaa Desemba 13, 2019

Nipashe

Messi ateseka na mzimu wa Liver mtoano Uefa




HABARI UK. 30

## Molinga aituliza Yanga, panga la wazawa laja

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Yanga leo ikitarajia kushuka Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma kuivaa Mwamgongo FC katika mechi ya kirafiki, uongozi wa klabu hiyo umesema utaendelea kuwafungashia virago wachezaji wote ambao hawajaridhishwa na viwango vyao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Dk. Mshindo Msolla alisema watabaki na wachezaji ambao wanaipa klabu faida na si vinginevyo.

"Rungu bado litaendelea kupita si kwa wachezaji wa kigeni tu bali hata wazawa, lengo ni kuwa na kikosi bora,"alisema.

Kuhusu sakata zima la kuachana na mchezaji Juma Balinya alisema wameachana naye kutokana na kutoridhishwa na kiwango chake uwanjani, katika michezo aliyoicheza tangu aanze kuichezea klabu hiyo.

Hata hivyo, licha ya awali mshambuliaji David Molinga kuwatia hofu mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kuwa naye anaweza kutumia nafasi ya kwenda kwao kusalimia kwa kutokomea huko moja kwa moja, ametuliza mzuka wao baada ya kubaki nchini na kuongozana na timu mkoani Kigoma.

Awali Molinga naye alielezwa kuwa miongoni mwa wachezaji walioandika barua kutaka kuvunja mkataba wake na klabu hiyo kwa madai ya kutolipwa mshahara wake kwa muda wa miezi miwili, hatua iliyozua hofu kwa mashabiki wa timu hiyo pamoja na uongozi ambao umeonyesha nia ya kutaka kuendelea kupata huduma yake.

Baada ya mechi hiyo ya leo, Yanga itashuka tena dimbani Jumapili kuivaa Mbao FC wakati huu ikijiandaa na mechi za Ligi Kuu pamoja na Kombe la FA.

Kwa mujibu wa mabadiliko ya ratiba yaliyotolewa na Bodi ya Ligi Kuu juzi, Desemba 24 Yanga itashuka Dimba la Sokoine mkoani Mbeya kuivaa Mbeya City kabla ya siku tatu baadaye kuivaa Tanzania Prisons katika uwanja huo.

MTAITAKA...




Kocha Mkuu mpya wa Simba, Mbelgiji Sven Ludwig Vandenbroeck (kulia), akiwa na msaidizi wake, Selemani Matola. **MPIGAPICHA WETU**

# KOCHA SVEN KUKUA NA VIATU VYAKE SIMBA SC

●●● Akusanya 'kijiji' Bunju mazoezini akiwasoma wachezaji, kumwaga sera zake leo kwa...

**Na Mwandishi Wetu**

ACHANA na maoni ya wadau wa soka walioanza kupuuza uwezo wa Kocha Mkuu mpya wa Simba, Mbelgiji Sven Ludwig Vandenbroeck, kutokana tu na umri wake mdogo, na mara moja mulika kauli ya uongozi wa klabu hiyo ambao unaamini utaendana na malengo yao.

Usiku wa kuamkia jana, uongozi wa Simba ulimtangaza Sven kuwa mrithi wa Mbelgiji mwenzake, Patrick Aussems aliyetimuliwa wiki mbili zilizopita kwa kile kilichodaiwa kushindwa kutekeleza malengo yake kwa timu hiyo kucheza soka la kiushindani na kujenga timu yenye nidhamu.

Hata hivyo Sven, aliyezaliwa Septemba 22, 1979 huku Vilvoorde, Ubelgiji, kwa sasa akiwa na miaka 40, wadau wengi kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwamo mitandao ya kijamii wanaamini atashindwa kuitendea haki klabu hiyo kongwe nchini.

Lakini baadhi kama ilivyo kwa uongozi wa klabu hiyo, wanaamini umri si tatizo na kwa soka la sasa makocha wengi vijana ndio wanaofanya vizuri na Simba inaweza kuwa sehemu sahihi ya yeye kuvivaa vema viatu vyake na kukua nayo akiwa hapo.

Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, akizungumzia hilo, alisema ni kocha kijana na mwenye malengo yanayofanana na klabu yao na kwamba mafanikio yake ni moja ya mambo yaliyoivutia klabu hiyo kumuajiri.

"Huyu ni Kocha kijana mwenye malengo yanayofanana na malengo ya klabu yetu, ameshashinda ubingwa wa Afcon akiwa Kocha Msaidizi wa Cameroon na ameshafundisha wachezaji wakubwa.

"Pia keshakuwa Kocha Mkuu wa Zambia na alikuwapo Kitwe mwaka jana tulipocheza na Nkana, anayajua malengo yetu na nini tunakitaka. Inshaallah Ijumaa [leo] ataongea na wanahabari kuelezea mipango na matarajio yake kwa machampioni wa taifa hili," alisema.

Katika wasifu wa Sven kisoka, mwenye kimo cha mita 1.81 (futi 5 na inchi 11), alicheza nafasi ya kiungo mkabaji nchini kwao Ubelgiji, kisha Uholanzi, Ugiriki na Norway akizitumikia Mechelen kati ya mwaka 1996-2000, Roda JC 2000-2004, De Graafschap 2004-2005, Akratitos mwaka 2005, Lierse 2006-2007, Vise 2007-2008 kabla ya kutundika daluga akiwa na Løv-Ham mwaka 2009.

Mbali ya Cameroon na Zambia pia aliinoa Klabu ya Niki Volou ya ugiriki mwaka 2014 inayoshiriki Ligi Daraja la Tatu kwa sasa, huku akisoma kozi nyingi mbalimbali za soka na utawala wake.

Mwaka 2017, Sven alikuwa Kocha Msaidizi wa Hugo Broos wakati alipoiongoza timu ya Taifa ya Cameroon kushinda Kombe la Mataifa ya Afrika, Afcon kabla ya Julai mwaka 2018 kutangazwa kuwa kocha wa timu ya Taifa ya Zambia 'Chipolopolo' lakini kutokana na kushindwa kuiwezesha kufuzu Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka 2019 nchini Misri, akatimuliwa.

Jana Sven, alihudhuria kwa mara ya kwanza kutazama mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika Uwanja wa Simba mo Arena, Bunju jijini Dar es Salaam na kukusanya nyomi ya mashabiki huku akifahamiana na benchi la ufundi likiongozwa na Kocha Msaidizi, Seleman Matola.

Hata, hivyo alikaa pembeni akiwasoma zaidi wachezaji waliokuwa wakiendelea na mazoezi uwanjani hapo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >